Alhamisi Agosti 22, 2024 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

# Nipashe

ISSN 0856 • Na. 0581776

www.ippmedia.com

MWANGA WA JAMII

The Guardian digital nipasheTZ nipasheTZ nipasheTZ 0745 700710

LIKE & FOLLOW US



**MBAPPE AIFUNGULIA KESI YA MADAI PSG**

UKURASA 21

UKURASA WA 3

**Biteko** akerwa makandarasi kuomba rushwa kuunganisha umeme



UKURASA WA 2

**Mwekezaji** apongeza Samia kuboresha sekta ya ufugaji

UKURASA WA 4

**Adaiwa** kumuua mke akimtuhumu kumroga akose nguvu za kiume

# Uchaguzi Mitaa wakwaa kigingi

- **Kesi** yafunguliwa Mahakama Kuu...

*Endelea Ukurasa 3*



Mohamed Mchengerwa



Bob Wangwe



Hamza Johari

## Atiwa mbaroni kisa mafuvu 17 ya binadamu kukutwa katika nyumba yake

UKURASA 19





Rais mstaafu, Dk. Jakaya Kikwete, akifurahia jambo na mwenyeji wake, Makamu wa Rais wa Nigeria, Kashim Shettima, walipokutana na kufanya mazungumzo katika Ikulu ya Rais, Abuja, jana. **PICHA: OFISI YA RAIS MSTAAFU**

UKURASA 2

**JK AIHAKIKISHIA NIGERIA UHUSIANO WA KIBIASHARA NA KIDIPLOMASIA**

**SAKATA 'BINTI WA YOMBO'**

## Wakili: Familia ya wanayemtaja "afande" kushtaki wanaomzushia

UK. 2

**MICHEZO** **YANGA, MAGOMA WATINGA KORTI KUU** UK.24

**MAONI,** UK.6

SAKATA 'BINTI WA YOMBO'

# Wakili: Familia ya wanayemtaja "afande" kushtaki wanaomzushia

**Na Jenifer Gilla**

FAMILIA ya Kamishna Msaidizi wa Polisi (SSP), Fatuma Kigondo, imesema inafikiria kufungua mashtaka dhidi ya waliosambaza kwenye mitandao ya kijamii kuwa ndugu yao amehusika kutuma vijana kumbaka na kumlawiti binti anayedaiwa mkazi wa Yombo Dovya, wilayani Temeke, mkoani Dar es Salaam.

Taarifa iliyotolewa na Mwanasheria wa Mahakama Kuu ya Tanzania, Emmanuel Muga, kupitia ukurasa wake wa X, ilieleza kuwa ndugu wa Askari polisi huyo waliwasiliana naye na kumweleza kusudio lao hilo, wakiwa na maelezo kuwa wanataka kuhakikisha haki inatendeka na ukweli wa jambo hilo unafichuliwa.

Alisema chanzo cha taarifa hiyo waliyoiita "ya kupotosha" ni mtu anayejitambulisha kama mshawishi wa mitandao ya kijamii na zinasambaa kwa haraka, ikiaminika kuwa ni ya kweli na kuisababisha familia hiyo kukosa amani.

Alisema familia hiyo ilimweleza kuwa SSP Fatuma siyo afande aliyezungumziwa kwenye video yenye utata inayosambazwa kwenye mitandao ya kijamii na kuwa ndugu yao ni ofisa wa polisi mwenye cheo cha SSP na si ASP kama ilivyodaiwa mtandaoni.

"Aidha, familia imethibitisha kuwa SSP Fatuma ni mjane na hana mume ambaye angeweza kuporwa kama ilivyosemwa," alisema.

Kuhusu washukiwa wa ubakaji, alisema familia imesema kuwa wamebainika wanatoka kwenye vikosi vingine visivyo chini ya amri ya SSP Fatuma, hivyo inawapa maswali kuwa ofisa huyo angewezaje kutoa maagizo kwa washukiwa hao, iwe ni kisheria au isivyo kisheria.

Alisema ndugu hao wamesikitishwa na tuhuma zinazoendelea kwenye mitandao ya kijamii dhidi ya ndugu yao na wangependa kutoa ufafanuzi kuwa hahusiki na madai hayo.

Alisema familia hiyo inasisitiza umuhimu wa umma kuwa na uwazi na kuchunguza kwa kina taarifa zinazozungumzwa kabla ya kuzipokea kama zina ukweli.

Akizungumza na Nipashe, Wakili Muga alisema, "Familia ya Fatuma wamenitafuta, amelalamika sana, anasema wanamchafua, pia yuko katika hali ya mshtuko na familia yake, hivyo wamenieleza kuwa wanafikiria kuchukua hatua za kisheria."

Tukio hilo liliibuliwa na aliyekuwa Meya wa Ubungo, Boniface Jacob wiki mbili zilizopita ambaye aliandika mkasa mzima kwenye ukurasa wake wa X huku akiwatumia nakala, Rais Samia Suluhu Hassan kama Amiri Jeshi Mkuu wa Majeshi Tanzania, Waziri wa Ulinzi wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dk. Stergomena Tax na Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum, Dorothy Gwajima.

Meya Boniface aliandika: "Binti huyu amebakwa na kulawitiwa akiwa anarekodiwa video tatu tofauti. Askari hao walimrekodi wakiwa wanambaka na kumlawiti, wamesambaza video zake mitandaoni kwa maagizo ya kiongozi wao (afande) ambaye amewatuma kumpatia huyu binti adhabu.



Rais wa Umoja wa Mabunge Duniani (IPU) na Spika wa Bunge, Dk. Tulia Ackson, akizungumza jambo na Rais wa Jamhuri ya Watu wa China, Xi Jinping, Ikulu ya China juzi. Wengine ni maspika wa mabunge mbalimbali wanachama wa IPU ambao walishiriki katika kikao maalum na Rais huyo. **PICHA: BUNGE**

# JK aihakikishia Nigeria uhusiano kibiashara, diplomasia

**Na Joyce Lameck**

RAIS mstaafu wa awamu ya nne, Jakaya Kikwete ameeleza utayari wa Tanzania kuimarisha uhusiano wake wa kibiashara, kidiplomasia na Nigeria.

Aidha, amesema anatambua umuhimu wa urafiki kati ya mataifa hayo mawili na kusisitiza dhamira ya Tanzania kuzidisha uhusiano huo.

Kwa mujibu wa taarifa kwa umma iliyotolewa jana, Kikwete aliyasema hayo juzi wakati wa mkutano kati yake na Makamu wa Rais wa Nigeria, Kashim Shettima, Ikulu ya Rais, Abuja.

Aidha, alisema anatambua jukumu la Chuo cha Ulinzi cha Taifa cha Nigeria katika kutoa mafunzo kwa wanajeshi wa Tanzania.

Alisema ushirikiano huo ni sehemu muhimu ya uhusiano wa ulinzi na kidiplomasia kati ya nchi hizo mbili, akieleza kuridhishwa kwa ushirikiano wa kina na mpana katika maeneo haya.

Makamu wa Rais wa Nigeria, Shettima, alitoa wito wa kuimarisha ushirikiano kati ya Nigeria na Tanzania, akisisitiza umuhimu wa ujumuishaji wa kikanda na juhudi za pamoja ili kufanikisha ukuaji na umoja wa bara.

Alisema nchi zote mbili zina uhusiano wa muda mrefu, hasa kama nchi za mstari wa mbele katika mapambano dhidi ya ubaguzi wa rangi na ukoloni.

Hata hivyo, alisisitiza haja ya kujenga historia hiyo ya pamoja ili kukuza uhusiano imara wa kiuchumi na kijamii, hasa ndani ya mfumo wa Eneo Huru la Biashara la Afrika (AfCFTA), "Tanzania ni moja ya hadithi za mafanikio za Afrika," alisema Shettima.

"Kuanzia Julius Nyerere hadi Samia Suluhu Hassan, Tanzania imebarikiwa kuwa na viongozi bora na kuwa taifa hilo ni mfano wa matumaini na utulivu katika Afrika Mashariki."

Makamu wa Rais wa Nigeria, alionesha furaha kwa kugundulika kwa akiba kubwa ya gesi, alisema Tanzania iko kwenye njia ya maendeleo ya haraka, jambo ambalo linafungua fursa za ushirikiano wa kina kati ya mataifa hayo mawili.

"Iwapo mataifa muhimu ya Afrika kama Nigeria na Tanzania yatapata mafanikio, bara zima litanufaika," alisisitiza.

Pia, aliipongeza Serikali ya Tanzania kwa kuunga mkono biashara za Nigeria zinazofanya kazi ndani ya mipaka yake, akitaja mafanikio ya kampuni kama United Bank for Africa, Guarantee Trust Bank na Dangote Group.

Alisema kuna uwezekano wa kuongezeka kwa biashara na uwekezaji kati ya nchi hizo mbili, jambo ambalo litazidi kuimarisha uhusiano wao wa kiuchumi.

# Mwekezaji ampongeza Rais Samia kuboresha sekta ya ufugaji

**Na Mwandishi Wetu, ZANZIBAR**

RAIS Dk. Samia Suluhu Hassan ameshiriki kutoa vyeti vya mafunzo ya Tamasha la Kizimkazi lililofanyika Uwanja wa Mwehe, Makunduchi, visiwani Zanzibar.

Katika tukio hilo, Rais alikabidhi vyeti kwa wahitimu wa mafunzo ya Kilimo Biashara, Ujasiriamali pamoja na Utalii.

Mkurugenzi wa Kampuni ya Unywaji na Uuzaji wa Maziwa nchini, Ahmed Asas, alipata nafasi ya kuzungumza namna fursa na manufaa watakayopata wana Kizimkazi kupitia kampuni yake ya Asas.

"Mheshimiwa Rais kuambatana na elimu hii si tu walipata elimu darasani, bali pia kama Asas tulileta ng'ombe wa maziwa wa kisasa pamoja na mbuzi wa nyama wa kisasa na kondoo ili wanafunzi waweze kujifunza kwa nadharia na vitendo," alisema.

Mkurugenzi Mtendaji huyo aliongeza: "Mheshimiwa Rais, zana ya mafunzo hayo ya mifugo ni kuwawezesha wafugaji wa Kizimkazi na viunga vyake waweze kufuga kisasa na kufuga kibiashara. Kama tunavyoelewa Zanzibar ina fursa kubwa sana na soko kubwa sana la nyama na maziwa.

"Lakini, bila kuwapatia wafugaji hawa elimu ya ufugaji wa kisasa na ufugaji wa mbegu bora ya ng'ombe, itakuwa vigumu sana kupata masoko ya bidhaa bora ya mifugo."

Alisema kuwa baada ya kuona mwamko ni mkubwa, wameshauriana na Kamati ya Maandalizi ya Elimu ya Kizimkazi, wanafunzi waliopata elimu ya mifugo, wataalikwa kwenda katika mashamba yao ya mkoani Iringa, kampuni yake itagharamia ziara yao hiyo.

Alisema lengo ni wajifunze mnyororo mzima kuanzia upandaji mifugo na namna ng'ombe wanavyokamuliwa hadi maziwa yanavyochakatwa kiwandani.

"Mheshimiwa Rais nikushukuru wewe binafsi na serikali yako kwa kuwezesha mazingira bora ya ufugaji, tumekuwa tunaona tasnia ya mifugo kila mwaka tunaweza kushindana na nchi jirani, na wafugaji wakubwa, wa kati na wadogo wamehamasika kufuga kisasa. Nikushukuru na kazi iendelee," alisifu Asas.

HABARI KITAIFA

# Biteko akerwa makandarasi wanaodai rushwa

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

NAIBU Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati, Dk. Doto Biteko amekerwa na tabia ya baadhi ya makandarasi wanaogeuka kuwa madalali wa kupiga dili na kudai rushwa kwa wananchi wakati wa kupeleka umeme kwenye vitongoji.

Biteko alisema hayo baada ya kushuhudia utiaji saini mikataba ya makandarasi 25 na Wakala wa Nishati Vijijini (REA) ambao umelenga kupeleka nishati ya umeme katika vitongoji 15 kwa kila jimbo isipokuwa majimbo ya Mkoa wa Dar es Salaam.

Alisema kumekuwapo na taarifa kuwa baadhi ya makandarasi wakati wa kutekeleza miradi ya kupeleka umeme vijijini waligeuka kuwa madalali wa kupiga dili na kuomba rushwa kwa wananchi.

"Kuna maeneo mengine unakuta makandarasi na watu wao wamegeuka kuwa madalali wa kupiga dili kwa wananchi. Mkandarasi anajua hapa nitapeleka umeme, lakini ama kibarua ama fundi wanapita kwa wananchi wanawaomba fedha."

"Ziko taarifa za makandarasi wetu wanapoenda kupeleka umeme vijijini wanao waomba fedha wananchi kwa fedha ambayo serikali imeshaitoa, kwamba ili nikusogezee nguzo kwako nipe kiasi hiki."

"Nataka niwaombe makandarasi wa REA, nikipata taarifa juu ya mkandarasi yeyote ambaye badala ya kufanya kazi ya kupeleka umeme ameingia kwenye dili la kutafuta fedha kidogo kwa Watanzania masikini ambao serikali imejinyima ili kuwapelekea umeme mimi sitashughulika na mkandarasi nitashughulika na wewe mtendaji wa REA kwa sababu lazima tufike mahali Watanzania wajue hii ni haki yao wanastahili kupata bila watu kutishwa na kuombwa rushwa, lazima tuwe watendaji wa watanzania ambao tuko daraja la juu tunaostahili kupata hizi huduma."

Pia, aliitaka REA kuendelea kusimamia makandarasi bila kuwaonea ili utekelezaji wa miradi ya umeme iende kwa kasi na kuhakikisha inafanya malipo kwa wakati kwa makandarasi ili aendelee kufanyakazi.

"Tukicheleweshana, tukaanza kufanya urasimu, mtu ameleta certificate mtu mmoja mahali fulani lazima mwonane ndio ulipwe hilo jambo kwanza linakera na kuudhi maana yeye ni mfanyabiashara na hakuja hapa kupiga picha." Alisema fedha zilizotengwa kutekeleza mradi huo ni nyingi na itakuwa ajabu zikija kufanyiwa tathmini wakute maelezo badala ya mradi kutekelezwa.

Awali, Mkurugenzi Mkuu wa REA, Hassan Saidy, alisema mradi wa kupeleka umeme kwenye vitongoji utahusisha makandarasi 25 ikiwa na thamani ya Sh. bilioni 363 kwa kila jimbo kupata vitongoji 15 isipokuwa kwa majimbo ya Mkoa wa Dar es Salaam.

Alisema mradi huo utatekelezwa kwa miezi 24 na hakutakuwa na kuongeza muda na kuhakikisha wanawashirikisha viongozi wa ngazi zote hatua ambavyo itaondoa migogoro.

Aliwataka makandarasi kuhakikisha vifaa vinashushwa kwenye vitongoji na kusisitiza kuwashirikisha wananchi pale wanapokata miti yao.

Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini, David Mathayo, alisema kamati inatoa rai kwa serikali kupitia Wizara ya Nishati kuhakikisha miradi hiyo inakamilika kwa wakati na kwa viwango vinavyokubaliwa.

Pia kuhakikisha miradi mingine inaendelea kutekelezwa na vitongoji vyote vinafikiwa na wananchi wananufaika na uwekezaji huo.



Makamu wa Rais, Dk. Philip Mpango, akipita katika daraja la zamani walilotumia wananchi wa Hurui, kuvuka katika mto uliopo kijijini kwao, baada ya kuweka jiwe la msingi la ujenzi wa daraja jipya la Hurui akiwa ziarani wilayani Mpwapwa, mkoani Dodoma jana. **PICHA: OMR**

# Uchaguzi wa Mitaa wakwaa kigingi

**Na Romana Mallya**

UCHAGUZI wa Serikali za Mitaa umekwaa kigingi: Mkurugenzi wa Jukwaa la Katiba Tanzania (JUKATA), Bob Wangwe na wenzake wawili wamefungua kesi kupinga mamlaka inayousimamia.

Kesi hiyo imefunguliwa Mahakama Kuu dhidi ya Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais - Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI) na Mwanasheria Mkuu wa Serikali (AG).

Bob na wenzake wanapinga uchaguzi wa serikali za vijiji, kamati za mitaa na wenyeviti wa vitongoji kusimamiwa na Ofisi ya Rais - TAMISEMI.

Kesi hiyo imepokewa Mahakama Kuu Kanda ya Dar es Salaam na imepangwa kutajwa leo mchana mahakamani huko na itakuwa mbele ya Jaji Wilfred Dyansobera.

Hivi karibuni, Chama cha ACT-Wazalendo nacho kilitangaza kusudio la kwenda mahakamani kufungua kesi ya kupinga TAMISEMI kusimamia uchaguzi huo ilhali Bunge lilishatoa uamuzi uchaguzi huo usimamiwe na Tume Huru ya Uchaguzi (INEC).

Azma hiyo ilitangazwa hivi karibuni na Makamu Mwenyekiti wa Taifa wa chama hicho, Tanzania Bara, Is-Haka Mchinjita, wakati akizungumza na wananchi jijini Tanga katika mkutano wa hadhara.

"Niwaambie ACT-Wazalendo tunajiandaa kufungua kesi wiki hii, tunaipeleka TAMISEMI mahakamani kuishtaki kwa kuwa wana nia ya kusimamia uchaguzi wakati kuna uamuzi wa Bunge ukielekeza INEC," alisema.

Julai 25 mwaka huu, katika ukurasa wake wa X, Katibu Mkuu wa CHADEMA, John Mnyika, pia aliandika: "...hatua zinazohitajika ni zilezile mbili baada ya waziri kutunga kanuni za uchaguzi ambazo ameanza kuzitumia:

"Mosi, kanuni hizo zipingwe mahakamani ili TAMISEMI izuiwe kusimamia uchaguzi badala yake, usimamiwe na Tume Huru ya Uchaguzi.

"Pili, maandalizi yaendelee katika kila mtaa, kijiji na kitongoji kukabiliana na wezi wa kura kwa nguvu ya umma."

Agosti 16 mwaka huu, Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais - TAMISEMI, Mohamed Mchengerwa, alitangaza tarehe rasmi ya uchaguzi huo kuwa ni Novemba 27 mwaka huu.

Vyama 18 kati ya 19 vyenye usajili wa kudumu nchini vilihudhuria tukio hilo la kutangazwa tarehe ya uchaguzi huo. CHADEMA haikupeleka mwakilishi katika tukio hilo.

Uongozi wa chama hicho ulisema haukushiriki tukio hilo kutokana na barua kuwafikia wakati Mwenyekiti wao Taifa, Freeman Mbowe na viongozi wengine waandamizi walikuwa wanashikiliwa na Jeshi la Polisi.


**NOTISI YA KULIPA DENI NA TANGAZO LA MNADA WA HADHARA**

Madalali tajwa hapo chini kwa idhini tuliyopewa na **Tujijenge Tanzania Financial Service Ltd,** tunatoa notisi ya siku kumi na nne (14) kwa wadaiwa kulipa madeni yao. Baada ya hapo hatua nyingine za kisheria zitachukuliwa ikiwa ni pamoja na uuzwaji wa mali walizoweka dhamana ya mikopo kama ilivyotangazwa gazetini

| Mdaiwa | Dhamana/ Mahali ilipo | Tarehe ya mnada | Dalali |
|---|---|---|---|
| Jerome Jerome Tesha | Plot ipo Utungemwago-Mkuranga | 06/09/2024 | RAPITECH SOLUTION LTD |
| Hamida Mohamed Alley | Plot ipo Tandika - Temeke | 06/09/2024 | RAPITECH SOLUTION LTD |
| William Patrick Chiboni | Gari T.656 DPB Toyota Land Cruiser Prado- Tabata SEPCO yard | 6/09/2024 | SEPCO DEBT COLLECTOR & AUCTIONEER CO. LTD |

**Masharti Mengine:**
Mnada utafanyika mahali dhamana ilipo kuanzia saa nne asubuhi. Mteja atalipa 25% siku ya mnada, 75% atalipa ndani ya siku 14, akishindwa kulipa 25% iliyolipwa hairudishwi na mnada utarudiwa tena. Gharama za kuona, kukagua, kuhamisha umiliki, kumtoa mdaiwa/mpangaji ni juu ya mnunuzi.

**Mawasiliano piga:**
**RAPITECH :0628866132/ 0755264606**
**SEPCO :0715683777/0750548337**
**Tujijenge (T) Financial Services Ltd: 0718068335**

HABARI KITAIFA


Beema Star INSURANCE

AUDITED FINANCIAL STATEMENTS 2023

STATEMENT OF PROFIT OR LOSS AND OTHER COMPREHENSIVE INCOME FOR THE YEAR ENDED 31 DECEMBER 2023

| Description | 2023 TZS'000 | 2022 TZS'000 |
|---|---|---|
| Insurance Revenue | 11,135 | 0 |
| Insurance Service Expenses | (3,488) | (4,500) |
| Net Expenses from Reinsurance Contracts | (53,913) | 0 |
| **Insurance Service Results** | **(46,266)** | **(4,500)** |
| Interest revenue calculated using the effective Interest Method | 156,871 | 4,688 |
| Net Impairment Loss on Financial Assets | 0 | 0 |
| **Investment Return** | **156,871** | **4,688** |
| Net Finance Income from Insurance Contracts | 0 | 0 |
| Net Finance Expenses from Reinsurance Contracts | 0 | 0 |
| **Net Financial Results** | **110,605** | **188** |
| Other Income | | |
| Other Operating Expenses | (212,245) | (464,225) |
| **Profit before Tax** | **(101,640)** | **(464,037)** |
| Income Tax Expenses | | |
| **Profit for the Year** | **(101,640)** | **(464,037)** |
| Other Comprehensive Income | | |
| **Total Comprehensive Income** | **(101,640)** | **(464,037)** |

STATEMENT OF FINANCIAL POSITION AS AT 31 DECEMBER 2023

| Description | 31.12.2023 TZS'000 | 31.12.2023 TZS'000 |
|---|---|---|
| **ASSETS** | | |
| Cash and Bank Balances | 46,222 | 5,648 |
| Financial Investments | | |
| Government Securities | 1,157,126 | 649,675 |
| Unlisted Securities | 98,587 | 49,016 |
| Current Tax Assets | 1,999 | 0 |
| Property and Equipment | 111,629 | 140,780 |
| **Total Assets** | **1,415,563** | **845,119** |
| **LIABILITIES** | | |
| Payables arising from Reinsurrance Arrangements | 182,185 | 132,656 |
| Insurance contract Liabilities | 180,324 | 151,586 |
| Other Payables | 14,739 | 2,800 |
| **Total Liabilities** | **377,248** | **287,042** |
| **EQUITY** | | |
| Share Capital | 1,200,000 | 1,200,000 |
| Retained Earnings | (750,655) | (1,230,893) |
| Other Reserves | 588,970 | 588,970 |
| **Total Equity** | **1,038,315** | **558,077** |
| **Total Equity and Liabilities** | **1,415,563** | **845,119** |

STATEMENT OF CHANGES IN EQUITY FOR THE YEAR ENDED 31 DECEMEBR 2023

| Description | Share Capital TZS'000 | Share Premium TZS'000 | Contingency Reserve TZS'000 | Retained Earnings TZS'000 | Total TZS'000 |
|---|---|---|---|---|---|
| As at 01 January 2023 | 1,200,000 | 16,139 | 572,831 | (1,230,893) | 558,077 |
| Restatement Amount | 0 | 0 | 0 | 581,878 | 581,878 |
| **Restated Balance of Prior Year** | **1,200,000** | **16,139** | **572,831** | **(649,015)** | **1,139,955** |
| Loss for the Year | | | | (101,640) | (101,640) |
| Transactions with Owners | | | | | |
| Transfer to Statutory Reserve | | | | | |
| **As at 31 December 2023** | **1,200,000** | **16,139** | **572,831** | **(750,655)** | **1,038,315** |

| Description | Share Capital TZS'000 | Share Premium TZS'000 | Contingency Reserve TZS'000 | Retained Earnings TZS'000 | Total TZS'000 |
|---|---|---|---|---|---|
| As at 01 January 2022 | 1,333,400 | 16,139 | 572,831 | (1,306,831) | 615,539 |
| Restatement Amount | (133,400) | | | 539,976 | 406,576 |
| **Restated Balance of Prior Year** | **1,200,000** | **16,139** | **572,831** | **(766,856)** | **1,022,115** |
| Loss for the Year | | | | (464,037) | |
| Transactions with Owners | | | | | |
| Transfer to Statutory Reserve | | | | | |
| **As at 31 December 2022** | **1,200,000** | **16,139** | **572,831** | **(1,230,893)** | **1,022,115** |

STATEMENT OF CASHFLOWS FOR THE YEAR ENDED 31 DECEMEBER 2023

| Description | 2023 TZS'000 | 2022 TZS'000 |
|---|---|---|
| **CASHFLOWS FROM OPERATING ACTIVITIES** | | |
| Loss for the Period | (101,640) | (464,037) |
| **Adjustments for:** | | |
| Charge/Release of Provision Charge for Impairment | 0 | 551,063 |
| Depreciation of Property and Equipment | 34,447 | 32,461 |
| **Operating Profit before Working Capital Changes** | (67,193) | 119,487 |
| **Changes in:** | | |
| Insurance contract Liabilities | 49,525 | 83,903 |
| Insurance Receivables | 0 | 6,320 |
| Other Receivables | (3,213) | (157,171) |
| Other Payables | 11,938 | |
| **Cash Generated from Operating Activities** | 58,250 | (66,948) |
| Payment of Lease liabilities interests | 0 | |
| Income Tax Paid | 0 | |
| **Net Cash generated from Operating Activities** | **(8,943)** | **52,539** |
| **CASHFLOWS FROM INVESTING ACTIVITIES** | | |
| Acquisition of Items of Property, Plant and Equipment | (5,296) | 0 |
| Proceeds from Sales of Equipment | | (173,241) |
| Investment in corporate bonds | (507,451) | (4,688) |
| Investment in Deposits with financial Institutions | (49,571) | 0 |
| **Net Cash Used in Investing Activities** | **(562,318)** | **(177,929)** |
| **CASHFLOWS FROM FINANCING ACTIVITIES** | | |
| Proceeds from Share Subscription | 611,835 | (133,400) |
| **Net Cashflow used in Financing Activities** | **611,835** | **(133,400)** |
| **Net Increase in Cash and Cash Equivalents** | 40,574 | (258,790) |
| Cash and Cash Equivalents as at the 01.01.2023 | 5,651 | 264,441 |
| **Cash and Cash Equivalents as at 31.12.2023** | **46,225** | **5,651** |

The financial statements were approved for issue by the Board of Directors and were signed on its behalf by:

Rose Ritte
**Chairperson**

Davis Rubagumya
**Director**


# Adaiwa kumuua mke akimtuhumu kumroga akose nguvu za kiume

**Na Grace Gurisha**

MAHAKAMA ya Hakimu Mkazi Kisutu, Dar es Salaam imeelezwa kuwa aliyekuwa Ofisa Usalama wa Taifa (jina tunalihifadhi kwa sababu za kisheria), anadaiwa kuingia makubalino na mganga wa kienyeji kumuua mke wake, Atwisege Kitalamo, kwa madai kuwa anamroga hadi anaishiwa nguvu za kiume.

Imedaiwa mahakamani huko kuwa, mganga huyo ambaye hakutajwa jina lake, aliagiza vijana wawili kwenda kufanya mauaji ya Atwisege kutimiza suluhisho la mwisho la matibabu ya mteja wake (50) aliyekuwa mgonjwa kwa wakati huo.

Hayo yalidaiwa jana na Hakimu wa Mahakama ya Mwanzo Mbagala, Debora William mbele ya Hakimu Mkazi Mkuu, Abdallah Mkama aliyepewa mamlaka ya kusikiliza kesi ya mauaji, wakati akisoma maelezo ya ungamo ya mshtakiwa huyo.

Debora, akisoma maelezo hayo ya ungamo aliyoyatoa mshtakiwa mbele yake huku akiongozwa na Wakili wa Serikali Mwandamizi, Deborah Mushi alidai kuwa mshtakiwa aliishi na mke wake kwenye ndoa tangu mwaka 2012.

Alidai kuwa, kwa kipindi hicho, kulikuwa na matukio mengi ya yanayodaiwa ya kichawi, yakimpata, akaona anayefanya hivyo ni mke wake Atwisege yaliyodumu kwa miaka tisa ya ndoa.

Ilidaiwa kwa kipindi hicho, ofisa huyo alikuwa akiumwa magonjwa mbalimbali, yakijumuisha kupooza mwili, kupungua nguvu za kiume na ngozi kutoka mwilini mwake, lakini kwa kipindi hicho alikuwa akimwuliza mke wake kama ni mchawi, naye (mkewe) alikana.

"Baada ya kumwuliza sana kwa muda mrefu, kuna siku Atwisege (marehemu) alimweleza kuwa, bibi yake mzaa baba ni mchawi sana, ikabidi aende kwa mganga wa kienyeji lakini matokeo yake alikuwa anapona, anaumwa tena.

"Marehemu alikuwa ana mpango wa kumuua, alishawahi kumwekea sumu kwenye soda akatapika, wakakubaliana na mganga kwamba matibabu ni Sh. milioni mbili akarudi kukaa nyumbani kwao wilayani Urambo," maelezo ya ungamo yaliyosomwa na Debora William. Shahidi huyo namba tatu wa upande wa mashtaka, Debora,aliendelea kusoma maelezo hayo kwamba Desemba 12, 2020, ofisa huyo alipigiwa simu na mganga kwamba anatakiwa kuongeza fedha Sh. milioni tatu, jumla ziwe Sh. milioni tano.

Ilidaiwa kuwa, mshtakiwa alimtumia mganga huyo Sh. 500,000 na kumwahidi kwamba akimaliza matatizo aliyoyapata ya msiba wa mke wake, atamalizia fedha zilizobaki. Baada ya mazishi, alimpigia simu mganga huyo na akatuma Sh. milioni 2.5 kwa njia ya wakala.

"Suluhisho la mganga la mwisho - alichukua vijana wawili kutoka Wilaya ya Urambo kwenda kufanya mauaji hayo. Baada ya kutekelezwa mauaji hayo, mganga alimpigia simu tena akimtaka aongeze fedha zitimie Sh. milioni 12 kwa sababu kazi ilikuwa ngumu," alidai.

Inadaiwa kuwa, mganga huyo alimweleza kuwa watu hao walikwenda nyumbani kwake wakiwa na bastola na wamemweleza kuwa asipotekeleza hilo watamfuata nyumbani kwake wamdhuru na yeye, akidai kuwa hana fedha kwa wakati huo.

Shahidi huyo aliendelea kusoma kuwa, mganga alimweleza ana magari mawili atayaweka rehani, akishapata fedha hizo atamrudishia. Baada ya muda kidogo, alipigiwa simu na mganga akashangaa anakamatwa.

"Aliitwa katika kituo chake cha kazi Oysterbay, ndipo akakamatwa," alidai Debora.

Shahidi huyo alidai kuwa, kipindi anachukua mshtakiwa maelezo ya ungamo, alikuwa Mahakama ya Mwanzo Magomeni na pia aliweza kumtambua mshtakiwa licha ya kwamba amekonda sana.

"Ninaweza kumtambua mshtakiwa (anataja jina lake) kwa sababu nilimchukua maelezo mimi kwa ukaribu, hapa mahakamani ninaweza kumtambua licha ya kwamba amekonda sana, alikuwa mtu kweli siku hiyo, alikuwa amevaa suti yake nyeusi ya Usalama wa Taifa," alidai.

Mbali na ofisa huyo, washtakiwa wengine ni Roger Shaban maarufu Mayala (25), na Furaha Ng'amba (47), wote ni wakazi wa Wilaya ya Urambo, mkoani Tabora.

Musho alidai kuwa washtakiwa wote wanashtakiwa kwa kosa moja la mauaji ya Atwisege. Inadaiwa kuwa Desemba 12, 2020 wakati wa usiku, washtakiwa Shabani na Ng'amba walivamia nyumba ya Atwisege na kumpeleka kwenye mto wa karibu na kumchinja hadi kufa, baada ya kuelezwa na mumewe kuwa anajihusisha na imani za kishirikina.



HABARI KITAIFA

## Uhusiano Tanzania, India kuimarisha biashara

**Na Romana Mallya**

TANZANIA imeomba Serikali ya India kuendeleza juhudi za biashara kati ya nchi hizo mbili ili kuimarisha uhusiano wa kibiashara uliopo.

Imesema kwa kufanya hivyo kutasaidia wafanyabiashara kunufaika na wanachofanya, kuongeza fedha za kigeni na fursa zaidi za uwekezaji.

Waziri wa Utamaduni, Sanaa na Michezo, Dk. Damas Ndumbaro, aliyasema hayo jijini Dar es Salaam wakati wa maadhimisho ya Miaka 78 ya Uhuru wa India yaliyofanyika katika Kituo cha Utamaduni cha Swami Vikekananda (SVCC).

Sherehe hizo zilihudhuriwa na mabalozi wanaowakilisha nchi zao nchini, wabunge, viongozi wa taasisi tofauti na diaspora wa India.

Akihutubia katika sherehe hizo kwa niaba ya Serikali ya Tanzania, Dk. Ndumbaro alisema India imeendelea kuwa mshirika mkuu wa Tanzania katika mauzo ya nje na hivi sasa, kiwango cha biashara kimeongezeka kwa kiasi kikubwa.

Alisema kwa mujibu wa takwimu za Tanzania, biashara baina ya nchi hizo mbili, imeongezeka kutoka Dola bilioni 1.6 mwaka 2020 hadi Dola bilioni 3.1 mwaka 2023.

Pia alipongeza Serikali ya India kwa kuendelea kusaidia Serikali ya Tanzania katika sekta mbalimbali, zikiwamo za maji na elimu.

Kwa mujibu wa Dk. Ndumbaro, mwaka 2022 kampuni sita kutoka India zilitia saini mkataba wa mradi wa maendeleo ya maji wenye thamani ya Dola milioni 5,000.

Alisema mradi huo utakapokamilika watu zaidi ya milioni nne watapata huduma ya maji safi na salama.

Balozi wa India nhini, Bishwadip Dey, alisema nchi hizo mbili zimefikia hatua muhimu katika uhusiano na kuboreshwa zaidi baada ya ziara ya Rais Samia Suluhu Hassan nchini India, iliyofanyika mwezi Oktoba mwaka jana.

Alisema biashara baina ya nchi hizo mbili iko katika mwelekeo mzuri, ambapo kiwango cha biashara mwaka 2023 kilifikia Dola bilioni 7.9, kulingana na takwimu za India.

Alisema kutokana hilo, Tanzania ni mshirika wa pili India kwa ukubwa wa kibiashara barani Afrika mwaka huu kutoka nafasi ya tatu mwaka jana.

Balozi huyo alisema kutokana na uhusiano mzuri ulioko, meli tatu za wanamaji wa India zilitembelea Tanzania mwaka huu na kushiriki kwa pamoja na Jeshi la Wanamaji la Tanzania katika mazoezi ya baharini.

Akizungumzia maadhimisho ya miaka 78 ya Uhuru wa India, Balozi huyo alisema, "Kama wengi wenu mnavyojua, India ilipata uhuru wake Agosti 15, 1947, na tangu wakati huo, imepiga hatua kubwa katika sekta mbalimbali.

Balozi huyo alisema kuwa chini ya uongozi wenye maono wa Waziri Mkuu wao, Narendra Modi, wamejiwekea lengo la kuwa taifa lililoendelea ifikapo 2047 na wamejitolea kuwezesha nchi yao na raia wake kujitegemea katika kila nyanja.

Kuhusu Tanzania, Balozi Dey alisema ina mandhari ya kuvutia, mbuga nyingi za kitaifa, fukwe safi, utamaduni mzuri, historia iliyojaa utajiri na watu wakarimu na hivi karibuni imekuwa kivutio kikubwa kwa watu mashuhuri wa India.

"Wakati ninaanza kutekeleza majukumu yangu, nina mpango wa kusafiri katika mikoa mbalimbali Tanzania, ili kushirikiana kwa dhati zaidi na wanajamii kuusogeza Ubalozi wa India karibu na Watanzania walioko nje ya Mkoa wa Dar es Salaam. Tumeamua kujipanga angalau kambi sita za kibalozi kote nchini kila mwaka," alisema.



Kiongozi Mkuu wa Kanisa Halisi la Mungu Baba Duniani, Baba Halisi (kulia), akimpongeza Diwani wa Kata ya Kunduchi, Michael Urio (kushoto), kwa kuchaguliwa na madiwani wa Manispaa ya Kinondoni kuwa Naibu Meya wa manispaa hiyo, alipomtembelea ofisini kwake, Dar es Salaam jana. **PICHA: IMANI NATHANIEL**

# Hatima kesi ya Kabendera na Vodacom kujulikana mwezi ujao

**Na Kulwa Mzee**

MAHAKAMA Kuu Masjala Ndogo Dar es Salaam inatarajia kutoa uamuzi Septemba 10, mwaka huu kama shauri la madai lililofunguliwa na Mwanahabari Erick Kabendera akiomba Kampuni ya mawasiliano ya Vodacom Tanzania iamuliwe kumlipa Sh. bilioni 28 kwa madai ilifanikisha kutekwa kwake, iko mahakamani kihalali au la.

Mahakama hiyo ilipaswa kutoa uamuzi huo jana, lakini iliahirisha mbele ya Jaji Salma Maghimbi kwa sababu haukuwa tayari na kupanga kusoma uamuzi Septemba 10, mwaka huu.

Julai 9, mwaka huu, akimwakilisha Kabendera, Wakili Peter Madereka alidai walalamikiwa Vodacom kupitia Wakili wao Gasper Nyika waliwasilisha majibu ya madai dhidi yao pamoja na kusudia la kupinga madai yaliyopo mahakamani.

Wakili Nyika alidai waliwasilisha majibu ya utetezi pamoja na pingamizi, walikubali pingamizi walilowasilisha lisikilizwe kwa njia ya maandishi.

Jaji Maghimbi aliamuru upande wa wajibu maombi kuwasilisha hoja za pingamizi Julai 23, mwaka huu.

Mwombaji alitakiwa kujibu pingamizi hilo Agosti 6, mwaka huu kama kuna hoja za nyongeza zilitakiwa kuwasilishwa Agosti 13 na Mahakama inatarajia kutoa uamuzi kama shauri hilo liko mahakamani kihalali au la leo. Vodacom kupitia Wakili Nyika wanapinga shauri hilo kusikilizwa kwa madai kesi ilifunguliwa nje ya muda kisheria wanaomba itupwe.

Katika kesi ya msingi, Kabendera anaomba mahakama hiyo iamuru kampuni hiyo imlipe fidia ya Dola za Marekani 10 milioni (sawa na Sh. bilioni 28 ), akiituhumu kuwa ndio iliyofanikisha kukamatwa kwake na askari polisi, tukio analoliita kutekwa na kisha kufunguliwa kesi ya uhujumu uchumi mwaka 2019.

Kabendera anadai kuwa kutokana na matukio hayo, amepata madhara ya kiuchumi na yasiyo ya kiuchumi, ya kijamii, maumivu ya kiakili na kimaono, hasara ya kutokufurahia maisha, hasara ya maendeleo binafsi na hadhi yake katika jamii na kutokuaminiwa kitaaluma.

Kabendera anataka kampuni hiyo imlipe Dola za Marekani milioni 10 kama fidia ya hasara halisi na riba kwa kiwango cha mahakama kuanzia tarehe ya hukumu mpaka kumaliza malipo yote.

Pia anataka alipwe fidia ya hasara ya jumla kadri mahakama itakavyotathmini, gharama za kesi na nafuu nyingine kadri mahakama itakavyoona inafaa.

Kwa mujibu wa hati ya madai katika kesi hiyo, Kabendera anaeleza matukio yaliyojiri katika simu yake kabla ya tukio la kukamatwa kwake, kuwa ilianza kupoteza mawasiliano na kumfanya ashindwe kupata huduma ya mawasiliano.

Kabendera pia ameelezea juhudi alizofanya kujua chanzo cha hali hiyo kwa kufanya mawasiliano na mwakilishi wa huduma kwa wateja na hata kutembelea ofisi za kampuni hiyo, lakini hakupata ufumbuzi wa tatizo hilo.

Katika hati ya madai, Kabendera anadai kuwa Julai 27, 2019, saa tisa alasiri, alipowasha simu yake ambayo alikuwa ameizima usiku wa siku iliyopita, ndipo alipobaini kuwa haikuwa na mtandao.

Anadai kuwa mwakilishi wa huduma kwa wateja wa Vodacom alimweleza kuwa namba yake ya simu ya Vodacom (+255767456796) ilikuwa na changamoto za kiufundi ambayo ilimhitaji kutoa taarifa katika kituo cha huduma kwa wateja cha karibu kilichoko Tegeta.

Kabendera alimtaka mwakilishi huyo kuelezea tatizo ni nini kabla ya kwenda kituoni huko, lakini mwakilishi huyo alikataa, akidai kuwa ni suala nyeti ambalo linamtaka aende binafsi kituoni huko.

Badala yake walimshauri atembelee ofisi zao zilizoko Mliman City asubuhi hiyo, hata hivyo saa tisa alasiri siku hiyohiyo ya Julai 29, 2019, ghafla simu yake ilianza kufanya kazi, kisha alipigiwa simu na mwakilishi wa Vodacom ambaye alimtaka (Kabendera) amweleze tatizo lake na baada ya Kabendera kumwelezea kwa takribani dakika tatu, alikata simu akiahidi kumpigia baadaye kidogo.

Anadai kuwa baada ya dakika tatu, alipokea simu iliyopigwa kutoka huduma kwa wateja Vodacom ambayo alipokea, akabaini kuwa ilikuwa ni sauti ya mwanamume, ambaye alimtaka Kabendera aeleze mahali alikokuwa na kwamba simu hiyo ilikuwa ikikwaruza kama vile ilikuwa inarekodiwa.

Anadai kabla ya simu hiyo kukatwa, Kabendera alimsikia aliyempigia simu akinong'ona kuwa alikuwa nyumbani kwake na kuongeza kuwa "sogea karibu na nyumba yake".

Kwa mujibu wa hati hiyo, maelezo hayo yalimshtua Kabendera na akakimbia sehemu ya juu ya nyumba yake ambako aliona magari kadhaa ambayo hakuyafahamu karibu na nyumba yake.

Kisha lilitokea gari lingine aina ya Toyota Alphard lililoegesha mbele ya magari hayo upande wa kulia mwa nyumba yake, wakashuka watu wanne ambao walijitambulisha kuwa maofisa wa Jeshi la Polisi lakini walikataa kutoa vitambulisho. Walimpiga pingu kumshikilia kizuizini kwa siku mbili.

Katika hati hiyo, inadaiwa kuwa wakati wa mahojiano, maofisa wa polisi walifika katika chumba cha mahojiano wakiwa na karatasi zilizochapishwa kutoka katika kompyuta za akaunti za fedha ya simu na namba za simu alizokuwa amezipiga kwa mwaka mzima.

Hivyo, walimhoji lengo la kila muamala aliofanya kwa mwaka mzima na pia uhusiano wake na watu aliokuwa amewasiliana nao miaka kadhaa.

Kabendera analalamika kuwa polisi na serikali walitoa taarifa kadhaa zenye mgogoro kwa umma kuhusiana na anachokiita "kutekwa" kwake na kwamba walimtuhumu kwa kutokuwa raia na kumkashfu Rais (wa wakati huo) John Magufuli.

Anadai alishtakiwa mahakamani kwa makosa ya utakatishaji fedha, uhujumu uchumi na ukwepaji kodi na matokeo yake walimweka chini ya ulinzi mkali katika mahabusu ya Gereza la Segerea.

Inadaiwa katika hati hiyo kuwa wakati akiwa mahabusu, mama yake, Verdiana Mujwahuzi alifariki dunia na hakuruhusiwa kuhudhuria mazishi yake na kwamba hata yeye mwenyewe alikuwa na tatizo kiafya.

Anadai katika hati hiyo kuwa kutokana na hali hiyo, aliamua kukiri makosa na kulipa fidia ya Sh. milioni 273 ili atoke mahabusu na kwamba baada ya kuachiliwa marafiki na familia yake walimweleza kuwa walipigiwa simu na polisi wakiwaonya kutokumtembelea mahabusu na kwamba vinginevyo wangepata hatari.

# MAONI & UCHAMBUZI

Nipashe
MWANGA WA JAMII

## Kodi lazima ilipwe kuleta maendeleo

**MAENDELEO** ya nchi hayawezi kupatikana bila kodi zinazokusanywa kutoka vyanzo mbalimbali vya mapato.

Ujenzi wa barabara za kisasa, hospitali, shule na huduma nyingine muhimu anazotakiwa kuzipata mwananchi zinatokana na kodi ambazo serikali inakusanya.

Hata hivyo, matokeo ya kodi hizo ni lazima yaonekane ili wananchi waendelee kuona umuhimu wa kulipa kama inavyoonekana katika nchi nyingine zilizoendelea duniani.

Katika nchi zilizoendelea kodi hizo pia husaidia kuwatunza wazee ambao hawawezi tena kujitegemea na badala yake kulelewa kwenye nyumba za kutunza wazee.

Hata kwa wale wanaoweza kujitegemea, serikali zao huwalipa kiwango fulani cha pesa kila mwezi ili waweze kununua mahitaji muhimu na kulipa bili mbalimbali za huduma.

Mara nyingi malalamiko hujitokeza wananchi wanapoona wanakatwa kodi, lakini fedha zinaelekezwa kwenye matumizi mengine ambayo hayawagusi moja kwa moja.

Vyanzo vya makusanyo ya kodi viko vingi na kama kila mwananchi angewajibika kuilipa nchi yetu ingekuwa mbali kimaendeleo.

Kwa nchi ambazo zimepiga hatua katika maendeleo, mengi yametokana na kodi zinazokusanywa na serikali.

Wananchi pia wanaelewa umuhimu wa kulipa kodi kwasababu wanaona faida zake katika kuwahudumia kwenye sekta mbalimbali.

Udanganyifu katika ulipaji kodi unarudisha maendeleo na kuifanya serikali kubeba mzigo mkubwa kutekeleza baadhi ya miradi kwa kutegemea ufadhili au mikopo kutoka kwenye nchi zilizoendelea.

Baadhi ya wafanyabiashara hudiriki kufanya udanganyifu kwenye ulipaji kodi kwa kuandika risiti zisizo za uhalisia na bidhaa walizomuuzia mteja.

Uaminifu kwa pande zote za ulipaji na ukusanyaji ni jambo muhimu sana ili kufikia hatua zilizofikiwa na nchi nyingine duniani zilizoendelea. Wakati mwingine uaminifu unakosekana kutokana na walipa kodi kuona fedha zao zinatumika vibaya kinyume na makusudio.

Rais Samia Suluhu Hassan, amekuwa akihamasisha wananchi kulipa kodi ili nchi iweze kusonga mbele na kukamilisha miradi ambayo imekwama kwa kukosa fedha.

Amekuwa akisisitiza kuwa ili nchi itekeleze miradi ya maendeleo wananchi hawana budi kulipa kodi zinazowekwa na serikali haijalishi ni ndogo au kubwa ili mradi iwe halali.

Tozo ndogo ndogo pia husaidia kwenye mapato na kujenga barabara, madaraja, shule na mambo mengine, kwa sababu hakuna serikali inayoendeshwa kwa pesa nyingine zozote isipokuwa pesa za kodi za wananchi wake.

Hata hivyo, miradi hiyo pia itunzwe ili iweze kudumu na kunufaisha vizazi vijavyo. Lakini, kuna baadhi ya wananchi hudiriki kuharibu miradi hiyo kwa makusudi na kusababisha hasara ya kuitengeneza tena badala ya kujenga miradi mingine.

Kuna ambao wana tabia ya kuchimba na kulima pembezoni mwa barabara na kusababisha mmomonyoko wa udongo na kuharibu miundombinu hiyo.


Kilometa moja tu ya barabara ni sawa na kujenga vituo vitatu vya afya vya kata pamoja na kuweka vifaa tiba ndani.

Kuna baadhi ya wanaohujumu miradi hiyo kwa kung'oa vyuma vya kingo vilizowekwa kwenye madaraja na kwenda kutengeneza vifaa mbalimbali. Ukiangalia gharama iliyotumika kutengeneza kingo hizo na vifaa vinavyotenezwa ni hasara kubwa. Wananchi hawafahamu sio serikali pekee inayoathirika bali hata wewe ambaye unalipa kodi.

Mara ngapi wananchi wanalalamika tozo zinazokatwa kwenye miamala ya simu, kama miundombinu itaendelea kuharibiwa hakuna shaka kuwa unafuu wa tozo hautakuwapo.

Ni muhimu kila mwananchi kuona uchungu na kuwa mlinzi wa mwenzake ili miradi inayojengwa iendelee kudumu na mingine ijengwe kwa lengo la kuleta maendeleo makubwa.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
**THE GUARDIAN LIMITED**
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko.** Dennis Ntaita. 0713 578284.
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0677-020701
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com




# Muungwana Lazima Nilonge

Na Mwandishi Wetu

## Lazima kusoma kwa tajiri, fukara

**AWALI** ya yote, ni vyema kufahamu ni aina gani ya usomaji unaozungumziwa hapa, hebu tujiulize maswali kadhaa: Ni kwanini watu wanasoma shule?

Kuna madhara gani yanaweza kuwapo kwa kukosa kusoma? Je, kila tajiri amesoma? Au, kila aliyefanikiwa kimaisha amesoma? Maswali hayo na mengine mengi yanaweza kupatiwa ufumbuzi, endapo tu tutajua, umuhimu wa elimu.

Inaweza kufasiriwa kuwa ni ufahamu au maarifa ayapatayo mtu, kutoka kwa mtu mmoja hadi mwingine.

Tukiangalia elimu ya Tanzania, ambayo imegawanyika katika vipindi vitatu, kabla ya ukoloni, wakati wa ukoloni na baada ya ukoloni mpaka sasa.

Tukumbuke kuwa kabla ya ukoloni elimu iliyotolewa ilihusisha zaidi vitendo, watu walifunzwa namna mfumo mzima wa maisha ulivyo, na kipindi hicho haikuhusisha maandishi mpaka yalipoletwa na wageni.

Wakati wa ukoloni, elimu ilitolewa na wageni mbalimbali kutoka nje. Wa kwanza kufika Tanzania walikuwa ni Waarabu wakifuatiwa na Wareno, Wajerumani kisha Waingereza. Kutokana na kupokezana huko kwa utawala kwa baadhi ya maeneo au nchi nzima, kila kundi lilibadili mfumo wa elimu kama kubadili mitaala na lugha ya kufundishia, vile vile malengo ya kutoa elimu, yalilenga matakwa yao bila kujali manufaa kwa Watanzania.

Lengo kubwa lilikuwa ni kupata watumishi, ambao wangetumika kutetea matakwa ya wakoloni. Kwa kipindi chao elimu iliyotolewa iliegemea nadharia zaidi.

Mfumo huo wa elimu umeleta athari kubwa sana kwenye elimu baada ya wageni kuondoka.

Baada ya ukoloni, elimu iliendelea kuwa ni ya kusoma na kuandika na kwa kiasi kidogo sana ilihusisha vitendo na mpaka sasa imebaki kuwa hivyo.

Hapa ndipo unaibuka mjadala kuwa, kusoma ni ngazi ya kwanza, lakini matumizi ya kilichosomwa ni ngazi muhimu.

Hivi sasa wasomi wamekuwa wengi na kila msomi anaamini kutendea kazi usomi wake kwa kupata ajira baada ya kuhitimu.

Fikra hizi ni za kizamani sana, kwa hali ilivyo sasa dunia haihitaji hivyo, bali elimu itolewayo itumike kwa vitendo. Maana yake nini?

Unachosoma kitoe mwangaza wa kuwaongoza watu katika njia iliyo sahihi, kwa hiyo utofauti wa wasomi na ambao si wasomi unaibuka hapa, kutokana na namna wanavyoyaendesha maisha yao.

Endapo mtu atakosa elimu hatakuwa na uwezo wa kutenda vizuri zaidi kama ambavyo angesoma kwanza.

Vijana wengi wamekuwa wakizua mijadala migi kuhusu matajiri ambao wamefanikiwa bila kusoma, mwisho wa mijadala hiyo huwa ni kuona hakuna maana yoyote kusoma.

Huku wakisahau kuwa, hata tajiri huyo anasaidiwa kuendesha biashara na mali zake huangaliwa na watu walioosoma ndiyo maana huajiri wasomi na wataalamu wenye weledi.

Kwa hapa Tanzania serikali imekuwa ikisisitiza kuhusu uchumi wa viwanda, kilimo cha kisasa, kujiajiri na ujasiriamali.

Utekelezaji wa yote hayo hauendani na idadi kubwa ya wasomi waliopo, kutokana na mfumo wa elimu ulivyo, kwa sababu ya kuegemea zaidi nadharia kuliko vitendo.

Ni changamoto hata katika fani nyingine kama mambo yanafanywa kwa ufanisi mdogo kutokana na ukosefu wa masomo yanayohusisha vitendo zaidi.

Ni vizuri kwa sababu serikali imelitambua hilo na kubadili mfumo wa elimu, unatarajiwa kuwa utaboresha wasomi na kupanua soko la ajira na kujiajiri pia.

Ili wasomi waanze kuzalisha vitu kwa ubora zaidi na kuwa na ufanisi katika kujiletea maendeleo.

Kwahiyo, kila mmoja anatakiwa afanye jitihada kutafuta elimu yenye manufaa, ili kuendana na mabadiliko ya sayansi na teknolojia.

Elimu inaweza kuwa na faida nyingine kama: kuwa njia bora ya kujenga taifa imara, kuongeza upeo na uwezo wa kufikiri kwa kutafuta maarifa zaidi na kuleta mabadiliko chanya.

Usiseme eti wasiosoma mbona wana hela unajidanganya vilevile kumbuka ndiyo ni nyenzo muhimu ya kutatua matatizo katika jamii.

Aidha, fahamu kuwa elimu haiwezi kuhamishika kwa maana kwamba leo unaweza kupata elimu halafu kesho ikapotea kichwani kwako, hivyo kusoma ni bora zaidi kuliko kusema Fulani hajasoma ni tajiri.

Tafuta elimu na maarifa usonge mbele na bila elimu hakuna maisha bora.

## Serikali Zanzibar kuweka mkazo kilimo cha mwani

**Na Mwandishi Wetu**

RAIS wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Dk. Hussein Ali Mwinyi, amesema Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar inakusudia kuweka mkazo zaidi kwenye sekta ya mwani ili kuzalisha bidhaa zenye ubora na kuzipatia soko la uhakika.

Dk. Mwinyi aliyasema hayo Ikulu, Zanzibar alipozungumza na Balozi wa Ulaya nchini, Tanzania, Christine Grau.

Alisema, asilimia 99 ya wakulima wa zao la mwani Zanzibar ni wanawake na kumweleza balozi huyo kuangalia haja ya kuwaunga mkono wanawake na wakulima wa mwani nchini hasa kwa mafunzo na vifaa vya kisasa ili wazalishe mwani wenye ubora utakaoenda sambamba na soko la uhakika.

Mbali na mambo mengine ya maendeleo na uwekezaji ikiwamo utalii, Rais Dk. Mwinyi pia alimweleza Balozi Grau kuwa uchumi wa buluu ni sera kuu ya uchumi wa Zanzibar na kumwomba kuangalia fursa zinazotokana na sera hiyo.

Pia, Rais Dk. Mwinyi ameupongeza Umoja wa Ulaya kwa ushirikiano mzuri na Tanzania na kusema kuwa wameshirikiana kwa miaka mingi kupitia sekta mbalimbali za maendeleo ikiwamo, elimu, maji, afya na miundombinu.

Balozi Christine, amesifu juhudi za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na kueleza kuwa wanafanyakazi kwenye maeneo mbalimbali ikiwamo kushirikiana na jamii kupitia serikali za mitaa na taasisi za kiraia (NGO's), kwenye masuala mbalimbali ya maendeleo na ustawi wa jamii Unguja na Pemba.

Alisema kupitia mradi wao wa "Green City" wamesaidia masuala ya jinsia hasa kuwawezesha wanawake kwenye elimu, uchumi ikiwamo uvuvi na masuala ya uongozi wa fedha.



Mwenyekiti wa Jumuiya ya Wazazi ya CCM Mkoa wa Lindi, Mussa Mkoyage, akizungumza wakati wa ziara ya Wajumbe wa Kamati ya Utekelezaji ya mkoa huo katika Kata ya Nanjilinji, juzi. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Mloganzila yawaita wenye shida ya magoti, nyonga

**Na Joseph Mwendapole**

HOSPITALI ya Muhimbili tawi la Mloganzila, imewataka Watanzania wenye shida ya magoti na nyonga kujitokeza kwa ajili ya kambi ya upasuaji kutoka kwa wataalamu wa ndani watakaoshirikiana na wabobezi kutoka India.

Kambi hiyo ya upasuaji, itakayoanza Agosti 26 hadi 30, itafanyika kwenye Hospitali ya Mloganzila na watu wenye matatizo ya aina hiyo watafanyiwa upasuaji.

Mkurugenzi Msaidizi wa Huduma za Upasuaji wa hospitali hiyo, Goodlove Mfuko, alisema watakaojitokeza watafanyiwa uchunguzi wa kina na kisha upasuaji kwenye kambi hiyo ambayo ni ya pili kufanywa na hospitali hiyo.

Alisema jana kuwa, maandalizi yote yamekamilika na kwenye kambi hiyo watashirikiana na mtaalamu kutoka hospitali kubwa nchini India ya Yashoda, Dk. Ram Mohan Reddy.

"Mtaalamu huyu atashirikiana na madaktari bingwa ambao ni wataalamu wa mifupa na ajali hapa Mloganzila, hii itakuwa mara ya pili kutoa huduma kama hii kwani mara ya kwanza tuliwafanyia upasuaji wa kubadilisha nyonga na magoti wagonjwa 170 kwa mafanikio makubwa," alisema.

"Kwa hiyo kwenye kambi hii ambayo ni ya pili tutashirikiana na daktari huyu mbobezi kutoka India kupata uzoefu ili tuweze kubadilishana naye uzoefu tuboreshe zaidi huduma zetu," alisema.

"Watu wenye matatizo ya nyonga na magoti wafike Mloganzila mapema ili wafanyiwe uchunguzi wa mapema kwa ajili ya kupewa hiyo huduma ya kubadilisha nyonga na magoti," alisisitiza Dk. Mfuko.

Naye daktari bingwa wa mifupa wa Mloganzila, Dk. Joseph Amos, ambaye amebobea kwenye upasuaji wa nyonga na magoti, alisema kambi hiyo itahusisha upasuaji wa magonjwa yote yanayohusisha nyonga na magoti.

"Tutakuwa na mtaalamu kutoka India ambaye ni bingwa wa upasuaji wa nyonga na magoti mwenye uzoefu wa miaka 20, atakuja na wataalamu wenzake hapa Mloganzila kufanya upasuaji huu," alisema.

Alisema Hospitali ya Mloganzila imeshaandaa mchakato unaoendelea kwa sasa wa kuwatambua watu wenye matatizo ya nyonga na magoti utakaoendelea mpaka Agosti 24 siku chache kabla ya kambi hiyo.

"Utambuzi huu unahusisha maumivu katika magoti, nyonga na watakapofika kwenye kliniki zetu watafanyiwa uchunguzi wa kina na wataalamu wetu waliobobea kwenye matibabu hayo. Tutawatambua ni wangapi watafanyiwa upasuaji na wangapi watafanyiwa matibabu ya kawaida," alisema Dk. Amos.

# Nchi 12 Afrika kuja kujifunza rada Tanzania

**Na Faustine Feliciane**

WATAALAMU wa masuala ya hali ya hewa kutoka katika nchi 12 za Afrika wanatarajia kuja Tanzania kupata mafunzo ya matumizi ya rada za hali ya hewa yatakayotolewa na Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania (TMA).

Akizungumza jana kwenye warsha ya waandishi wa habari kuelekea kwenye utabiri wa msimu wa mvua za vuli, Kaimu Mkurugenzi wa TMA, Dk. Ladislaus Chang'a, alisema mafunzo hayo yatakayoanza Agosti 26- 30 yatatolewa kwa ushirikiano na Kitengo cha Elimu na Mafunzo cha Mamlaka ya Hali ya Hewa Duniani (WMO) ili kuwajengea uwezo wataalamu wa hali ya hewa katika nchi za Afrika kuhusu matumizi ya rada hizo.

"Mafunzo haya yatafanyika jijini Mwanza maeneo ambayo wataalamu watajifunza kwa vitendo kutokana na uwepo wa rada hizo," alisema Dk. Chang'a.

Alizitaja nchi zitakazotoa wataalamu kuwa ni Kenya, Rwanda, Burundi, Uganda, Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo, Malawi, Comoro, Msumbiji, Mauritius, Shelisheli na Sudan Kusini.


"Fursa hizi za kuandaa mafunzo haya zinatokana na juhudi za serikali katika kuwekeza kwenye miundombinu na vifaa vya hali ya hewa, ukanda wa Afrika Mashariki tumekuwa nchi kinara kwenye miundombinu na vifaa," alisema Dk. Chang'a.

Alisema mpaka mwakani serikali itakuwa imekamilisha ujenzi wa rada saba za hali ya hewa na kuwa miongoni mwa nchi zenye rada nyingi Afrika.

Katika hatua nyingine, Mamlaka hiyo leo inatarajiwa kutoa utabiri wa mvua za vuli maalum kwa kipindi cha mwezi Oktoba, Novemba na Desemba (OND).

## KABWELA

FADHILI MOHAMED




HABARI PICHA

# TAFRIJA YA KUWAAGA MKURUGENZI WA BIASHARA NA MENEJA UENDESHAJI WA KAMPUNI YA THE GUARDIAN LTD KATIKA PICHA



Mwenyekiti Mtendaji wa IPP Ltd, Abdiel Mengi (wa pili kulia), akiwa katika picha ya pamoja na Mkurugenzi wa Biashara wa Kampuni ya The Guardian Ltd (TGL), Ajay Goyal (shati jekundu) na Meneja Uendeshaji, Murugan Vajran (wa pili kushoto) na familia zao, wakati wa tafrija ya kuwaaga baada ya kumaliza muda wao, iliyofanyika Dar es Salaam juzi. **PICHA ZOTE: MPIGAPICHA WETU**



Mwenyekiti Mtendaji wa IPP Ltd, Abdiel Mengi, akiwa pamoja na familia ya Murugan Vajran na mkewe, Gowri Murugan na mtoto, Thanish, wakati wa tafrija hiyo.



Mwenyekiti Mtendaji wa IPP Ltd, Abdiel Mengi, akiwa pamoja na familia ya Ajay Goyal na mkewe, Ritu Goyal wakati wa tafrija hiyo.



Familia zinazoagwa zikiwa katika picha ya pamoja na Mwenyekiti Mtendaji wa IPP Ltd, Abdiel Mengi, Naibu Meneja Mkuu wa Kampuni ya TGL, Jackson Lema na wakuu wa idara mbalimbali za kampuni hiyo.



Naibu Meneja Mkuu wa Kampuni ya TGL, Jackson Lema (wa nne kulia) na baadhi ya wakuu wa idara wakiwa katika picha ya pamoja na familia zinazoagwa.



Mhariri Mtendaji wa gazeti la Nipashe, Beatrice Bandawe (kushoto), akikabidhi zawadi maalum kwa Ajay Goyal na mkewe, Ritu Goyal

## Waziri achangia mil. 10/- KKKT

**Na Allan Isack,** SIMANJIRO

WAZIRI wa Madini, Anthony Mavunde, ametoa mchango wa Sh. milioni 10 kwa Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania (KKKT), Dayosisi ya Kaskazini Kati.

Waziri Mavunde alichangia kiasi hicho wakati wa ibada ya uzinduzi wa usharika mpya wa kanisa hilo wa Songambele uliopo Mamlaka ya Mji wa Mirerani wilayani hapa Mkoa wa Manyara iliyongozwa na Askofu wa KKKT Dayosisi ya Kaskazini Kati, Dk. Godson Mollel.

Akizungumza kwenye harambee iliyoendeshwa wakati wa uzinduzi huo, Waziri Mavunde, aliwapongeza wadau walioshiriki na kuchangia ununuzi wa eneo la kanisa hilo.

Aliwataka wananchi kuwa na utamaduni wa kushiriki kuchangia shughuli za Mungu na siyo kujihusisha na mambo ya duniani pekee, ikiwemo harusi.

Askofu Mollel, aliwataka waumini kuwa na upendo katika maisha yao.

Mkuu wa Wilaya ya Simanjiro, Fakii Lulanda, alimpongeza Mavunde kwa kushiriki katika utekelezaji wa miradi ya maendeleo.

Mbunge wa Bunge la Afrika Mashariki (EALA), James Ole Millya, alitoa ushauri kwa KKKT kuomba na kumiliki maeneo mengi hasa ya vijijini kwa manufaa ya miaka ijayo.

Mchungaji Kiongozi wa Usharika huo, Sion Mollel, alisema Songambele wenye mitaa mitano, ulianzishwa Januari Mosi mwaka jana chini ya Mchungaji Loishiye Godson Laizer.

## Wanafunzi wapatiwa elimu ufugaji nyuki

**Na Cynthia Mwilolezi,** ARUSHA

MKUU wa Wilaya ya Monduli mkoani hapa, Festo Kiswaga, amewataka wanafunzi wa Shule ya Msingi Mswakini kutumia elimu ya ufugaji nyuki kuziingizia kipato familia zao.

Kiswaga alitoa wito huo jana katika shule hiyo, wakati akizindua darasa moja lililojengwa kwa zaidi ya Sh. milioni 32 na Kampuni ya Utalii ya The Singing Grass kwa lengo la kukabiliana na upungufu wa madarasa uliopo shuleni hapo.

Alisema ufugaji nyuki ni biashara nzuri na kila aliyeanzisha mradi huo hajutii kwa kuwa ina manufaa kiuchumi.

Kaswaga, alishukuru kampuni hiyo kwa kuunga mkono juhudi za serikali kwa kujenga darasa hilo lenye ubora kwa kuwa litaongeza chachu ya watoto kusoma.

Mwenyekiti wa Kampuni hiyo, Mahfuj Munshi, alisema katika kuhakikisha shughuli za jamii zinaendelea kwa ustawi wa eneo hilo, linalozunguka Hifadhi ya Taifa ya Tarangire, wamekubaliana kuwasaidia kwenye faida zao wanazopata.

Mshauri wa Kampuni hiyo, Nicephor Lesio, alisema lengo la kuanzisha mradi wa ufugaji nyuki ni kuinua uchumi wa shule hiyo na kusambaza elimu kwa jamii ya eneo hilo.

Mkuu wa Shule hiyo, Yesaya Meiyan, alishukuru kampuni hiyo kwa misaada inayowapata kwa kuwanufaisha wanafunzi 707 shuleni hapo na kununua baadhi ya mahitaji kutokana na kipato cha ufugaji nyuki.

# Wafanyabiashara wanawake, wajasiriamali wapewa somo

**Na Cynthia Mwilolezi,** ARUSHA

NAIBU Spika wa Baraza la Wawakilishi Zanzibar, Mgeni Hassan Juma, amewataka wafanyabiashara wanawake na wajasiriamali nchini kulinda biashara zao kwa kukata bima.

Juma alitoa rai hiyo jana jijini hapa mbele ya Mshauri wa Rais na Mwenyekiti wa Kamati ya Jukwaa hilo Kitaifa, Angellah Kairuki, wakati wa ziara yao ya kujionea jitihada zilizofanywa katika uwezeshaji wanawake kiuchumi na wasichana.

"Nimefarijika sana kuona jinsi mabaraza ya uwezeshaji wa wanawake kiuchumi katika mkoa huu yanavyofanya kazi nzuri ya kuwaunganisha wanawake kiuchumi, niwaombe mkate bima ili kulinda biashara zenu ziweze kuwa salama muda wote," alisema.

Alisema licha ya kuonyesha uthubutu wa kufanya biashara, bado wanakabiliwa na ukosefu wa mitaji, elimu ya biashara na fedha, hivyo mabaraza hayo yanatakiwa kuongeza juhudi kuwaunganisha kupata mikopo na elimu ya fedha.

"Mkipata mikopo na elimu ya fedha hasa kwa wajasiriamali nina imani biashara zenu zitakuwa na fursa za masoko kwa kuwa takwimu zinaonyesha bado nchi yetu ipo chini kupeleka bidhaa nje," alisema Juma ambaye ni Makamu Mwenyekiti wa Kamati ya Jukwaa la Kizazi chenye Usawa.

Kwa upande wake, Kairuki, aliwataka wanawake wafanyabiashara na wajasiriamali kutumia maonesho kutangaza bidhaa zao na kupanua wigo ndani na nje ya nchi.

"Pia jisajilini kwenye vikundi muweze kupata mitaji kupitia mikopo ya asilimia 10 ambayo itaanza kutolewa hivi karibuni na halmashauri zetu nchini bila riba," alisema.

Alitoa rai kwa wanawake wa Mkoa wa Arusha kuchangamkia fursa zilizoko katika maeneo yao ikiwamo ya utalii kwa kuwa zinatoa fursa kwa wao kufanya biashara.

Naibu wa Benki Kuu Tanzania (BoT), Sauda Msemwa, alisema imetenga fedha za kukopesha taasisi ndogo kutoka asilimia 50 hadi 70 kupitia baadhi ya benki nchini zinazodhamini na serikali.

Awali Mwenyekiti wa Baraza la Uwezeshaji Wanawake Kiuchumi Mkoa wa Arusha, Sifa Swai, aliiomba serikali kuliwezesha kuwafikia wanawake katika wilaya za pembezoni.

Katika ziara hiyo, wajumbe wa kamati hiyo, walikutana, kujadiliana na Jukwaa la Wafanyabiashara na Wajasiriamali na kutembelea Kituo cha Taifa cha Kuhifadhi Kumbukumbu za Utafiti wa Masuala ya Wanawake kilichoko Chuo cha Maendeleo ya Jamii Tengeru.



Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar na Mlezi wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) Mkoa wa Tanga, Hemed Suleiman Abdullah (wa pili kushoto), akisalimiana na Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya ya Muheza, Erasto Mhina, alipowasili kwa ajili ya kuzungumza na viongozi wa chama na serikali wilayani humo, hivi karibuni. **PICHA: STEVEN WILLIAM**

# Wanafunzi wachanganywa madarasani, kisa moto

**Na Steven William,** MUHEZA

VYUMBA viwili vya madarasa ya Shule ya Msingi Mkumbi iliyopo Kijiji cha Tanganyika Kata ya Lusanga wilayani hapa Mkoa wa Tanga vimeteketea kwa moto na kusababisha wanafunzi wake kulazimika kuchanganywa madarasani mengine wakati wa masomo.

Hayo yamebainika kwenye kikao cha baraza la madiwani wa halmashauri hiyo kilichokutana kujadili kero zinazowakabili wananchi katika kata zao kilichofanyika wiki iliyopita.

Ofisa Elimu wa Shule za Msingi wa Halmashauri ya Wilaya ya Muheza, Pili Maximilian, alisema moto huo umeteketeza darasa la awali, la saba na madawati yapatayo 50.

Mkurugenzi wa halmashauri hiyo, Dk. Jumaa Mhina, alikiambia kikao hicho kuwa wameanza uchunguzi ili kubaini chanzo cha moto huo.

Mhina, alisema halmashauri hiyo inafanya jitihada kutafuta fedha za kukarabati madarasa hayo na kununua madawati ili wanafunzi warejee kuendelea na masomo yao na kuondokana na msongamano na usumbufu wakati wakifundishwa na walimu wao.

Diwani wa Magila, David Kilua, Diwani wa Makole, Shaban Achimwene na Diwani wa Kicheba, Hamis Mkodingo, walisema wamemshauri mkurugenzi wa halmashauri hiyo kutafuta fedha ili madarasa hayo yakarabatiwe haraka na kuwaondolea kero wanafunzi wa madarasa hayo.

Diwani wa Lusanga, Anthony Kabulwa, ilipo shule hiyo, alitembelea madarasa hayo na kujionea uharibifu uliosababishwa na moto huo.

Kabulwa, alisema kutokana na moto huo kusababisha upungufu wa madarasa hayo, wanafunzi wa darasa la tano wanachanganywa na wa la sita na wa awali na la kwanza.

Alisema hali ya madarasa la kwanza, nne na tano nayo ni mbaya kutokana na kuvuja wakati wa mvua, hivyo yanahitaji kufanyiwa ukarabati haraka iwezekanavyo.





# Wachimbaji wadogo kinara kutorosha madini nchini

**Na Shaban Njia,** KAHAMA

WAZIRI wa Madini, Antony Mavunde, amesema wachimbaji wadogo wa dhahabu wilayani hapa Mkoa wa Shinyanga wanaongoza kwa utoroshaji wa madini nchini na kuikosesha serikali mapato kwa kushindwa kutoza kodi.

Mavunde alitoa kauli hiyo jana kwenye kikao kazi cha kupokea Ripoti ya Benki ya CRDB ya utekelezaji wa kutoa huduma za fedha kwa wachimbaji wadogo na utoaji wa mikopo kwa wachimbaji wa madini.

Alisema kitendo cha wachimbaji hao kimeilazimu wizara yake kuunda kikosi kazi maalum cha kupambana na utoroshaji wa madini ili kukomesha tatizo hilo.

Alionya kuwa, wachimbaji wanaowakamata wanachukuliwa hatua kali ikiwa ni pamoja na wizara hiyo kuwafutia leseni zao moja kwa moja.

Mavunde, aliwataka wachimbaji na wafanyabiashara kuzingatia sheria na kufuata utaratibu kwa kuuza madini wanayopata katika masoko yaliyopo kila mikoa.

Ofisa Biashara Mkuu wa CRDB Makao Mkuu, Boma Raballa, alisema wanaendelea kutoa mikopo ya vifaa vya uchimbaji na fedha kwa masharti nafuu kwa wachimbaji wadogo na wale wa kati nchini kwa lengo la kuwaondolea vikwazo katika uzalishaji.

Mkuu wa Mkoa wa Shinyanga, Anamringi Macha, alisema mikopo hiyo inawasaidia wachimbaji kuongeza uzalishaji na mapato kwa serikali.

Anamringi aliwasihi wachimbaji hao kutumia mikopo hiyo kwa malengo yaliyokusudiwa.

Mwenyekiti wa Chama cha Wachimbaji Wadogo Mkoa wa Shinyanga (SHIREMA), Hamza Tandiko, alisema moja ya changamoto iliyokuwa inawakabili katika uzalishaji ni vifaa na rasilimali fedha.

Tandiko alisema mkopo walioupata wa Sh.bilioni 10 watautumia vema ili kufikia malengo.



Mkurugenzi Mtendaji wa Chama cha Waandishi wa Habari Wanawake Tanzania (TAMWA), Dk. Rose Reuben, akitoa mafunzo ya kuwaongezea uzoefu waandishi wa habari pamoja na maofisa uhusiano kutoka taasisi binafsi, yaliyoandaliwa na Taasisi ya Aga Khan, jijini Arusha jana. **PICHA: WOINDE SHIZZA**

# Vifo vya mifugo vyatikisa Shinyanga

**Na Marco Maduhu,** SHINYANGA

BARAZA la Madiwani wa Halmashauri ya Wilaya ya Shinyanga mkoani hapa, limeshtushwa na kukithiri kwa vifo vya mifugo na kuiomba serikali kuingilia kati ili kunusuru uchumi wa familia za wafugaji na Taifa.

Ombi hilo limetolewa na Mwenyekiti wa baraza hilo, Ngassa Mboje katika kikao chake kilichofanyika mapema wiki hii baada ya kujadili taarifa iliyowasilishwa ya kukithiri kwa vifo vya mifugo hiyo.

Mboje alisema kukithiri kwa vifo vya mifugo kunatishia hali ya uchumi na maisha ya familia za wafugaji na kuiomba serikali kupitia Wizara ya Mifugo iingilie kati ili kunusuru tatizo hilo.

"Mimi nina ng'ombe 100, nusu wamekufa na wananchi kila siku wanalia mifugo kufa na hatujui ni ugonjwa gani, kadhalika imani potofu zimeanza kuzagaa kuwa huenda chanjo ya mifugo ndiyo tatizo, tunaomba serikali itunusuru kwa hili," alisema Mboje.

Alisema uchumi wa wananchi katika halmashauri hiyo unategemea kilimo na mifugo, na kwamba vifo hivyo vina athari kubwa kwao, halmashauri na taifa kwa kukosa mapato.

Ofisa Kilimo, Mifugo na Uvuvi wa Halmashauri hiyo, Edward Maduhu, alithibitisha kutokea kwa vifo na kutoa taarifa kwa waratibu wa magonjwa ya mifugo Kanda ya Ziwa waliopo jijini Mwanza ili wafike kufanya uchunguzi kubaini chanzo cha vifo hivyo.

Baadhi ya wafugaji wameiomba serikali kuwanusuru kwa kuwa wameporomoka kiuchumi kutokana na mifugo yao yote kufa.

# Walimu wabanwa ufaulu wanafunzi

**Na Vitus Audax,** MWANZA

WALIMU wa Mkoa wa Mwanza wametakiwa kuwajibika kwa bidii na kupandisha matokeo kwa wanafunzi wa madaraja ya kwanza hadi la tatu ili kutimiza malengo ya mkoa huo.

Rai hiyo imetolewa na Ofisa Elimu Mkoa huo, Martin Nkwabi, juzi wakati wa kutangazwa kwa matokeo ya utamilifu kidato cha nne kwa Mikoa ya Kanda ya Ziwa ambayo ni; Geita, Simiyu, Kagera, Mara na Mwanza.

Kwa mujibu wa Nkwabi, malengo ya mkoa huo ni kuhakikisha wanafuta daraja sifuri na kupunguza la nne kwa wanafunzi.

Alifafanua kuwa malengo ya mitihani hiyo si kujikita tu kuona mwanafunzi amefeli au amefaulu, bali ni kujipima kwenye ufundishaji wa walimu ili kurekebisha kasoro na kufanya vizuri kwenye mitihani wa mwisho ya kuhitimu elimu ya sekondari.

Akitangaza matokeo hayo, Kaimu Katibu Tawala wa Mkoa huo, Emily Kasagara, alisema ufaulu wenye tija daraja la kwanza hadi la tatu ni asilimia 26.48 na kujikita katika daraja la nne kwa asilimia 13.01 huku sifuri ikiwa ni asilimia 9.02.

Kasagara, aliwataka walimu hao kuwajibika ili kupandisha ufaulu hususani madaraja ya kwanza, pili na tatu.

"Mkoa wa Mwanza umeongoza kwa ufaulu asilimia 86.13 ikifuatiwa na Simiyu. Tunazipongeza halmashauri za Manispaa ya Ilemela, Jiji la Mwanza na Bukombe kwa kufanya vizuri," alisema Kasagara.

Alisema Serikali itaeendelea kuimarisha miundombinu kwa kukarabati shule kongwe, kujenga mpya na kuongeza miundombinu ya madarasa, mabweni, maabara na vyoo.

# Wanakijiji 6,000 wapata majisafi

**Na Vitus Audax,** TABORA

ZAIDI ya wakazi 6,000 wa Kijiji cha Kigandu, Kata ya Mwakashanhala Wilaya ya Nzega mkoani hapa wameanza kunufaika na huduma ya majisafi.

Hayo yalibainishwa juzi na Meneja wa Wakala wa Maji na Usafi wa Mazingira Vijijini (RUWASA) wilayani hapa, Mhandisi Gaston Ntulo, wakati akitoa taarifa ya utekelezaji wa mradi wa maji kwa Kiongozi wa Mbio za Mwenge wa Uhuru Kitaifa mwaka huu, Godfrey Mnzava.

Ntulo, alisema mradi huo uliogharimu zaidi ya Sh. milioni 600 umemaliza kilio cha muda mrefu kwa wakazi wa kijiji hicho cha kukosa maji kwa muda mrefu na kusababisha wanawake na watoto kutumia muda mrefu kusaka huduma hiyo mbali na maeneo wanayoishi.

Alisema mradi huo ambao ni sehemu ya upanuzi wa mradi wa maji kutoka Ziwa Victoria, ulianza kutekelezwa Aprili 12, mwaka jana na kukamilika Mei 16, mwaka huu na kwamba umekamilika kwa asilimia 100 na upo kwenye muda wa matazamio.

Akizungumza baada ya kukagua na kuzindua mradi huo, Mnzava, alisema mradi huo ni matokeo ya kazi nzuri inayofanywa na Rais Samia Suluhu Hassan ya kumtua mama ndoo ya maji kichwani.

Aliwataka wananchi kuendelea kutunza mazingira na kulinda vyanzo vya maji ili kukabiliana na tatizo la kukosa maji kutokana na ukame katika maeneo yao.

**Ntulo, alisema mradi huo uliogharimu zaidi ya Sh. milioni 600 umemaliza kilio cha muda mrefu kwa wakazi wa kijiji hicho cha kukosa maji kwa muda mrefu na kusababisha wanawake na watoto kutumia muda mrefu kusaka huduma hiyo mbali na maeneo wanayoishi.**

ama
ALHAMISI AGOSTI 22, 2024
AFYA NA MAZINGIRA



Ukurasa 12

**Shirika na mchakamchaka wa elimu ya uzazi kwa vijana**



**Inaelezwa ni raha kujifungulia ndani ya maji ya jakuzi**

Ukurasa 14

# Imani hizi potofu zinavyowanyima watoto haki ya kunyonya, wakianzishiwa vyakula mapema

**Na Shaban Njia, KAHAMA**

LICHA ya wataalamu wa afya kusisitiza ulazima wa kunyonyesha mtoto miezi sita ya mwanzo bila kulishwa chochote, wapo wanawake wanaoogopa jukumu hilo wakitoa utetezi wa mila na desturi zinazopotosha.

Ni wenye mtazamo kuwa maziwa ya kwanza baada ya kujifungua yenye rangi ya njano si salama kwa mtoto, hivyo yakamuliwe chini mpaka yanapobadilika rangi na kuwa meupe.

Kwa mujibu wa matokeo ya utafiti wa afya ya uzazi na mtoto pamoja na viashiria vya malaria wa mwaka 2022, kitaifa watoto walionyonyeshwa maziwa ya mama pekee kipindi cha miezi sita ya mwanzo ilikuwa ni asilimia 64 na walionyonya hadi miaka miwili ni asilimia 37.3 pekee.

Kadhalika Shinyanga, inatajwa na ripoti hiyo kuwa watoto walionyonya maziwa ya mama pekee ilikuwa asilimia 50 huku wengine waliobaki wamenyonyeshwa kwa kipindi cha miezi sita na kuanzishiwa vyakula mbadala kama maziwa ya wanyama na uji.



Mama anaelekezwa na Wizara ya Afya anyonyeshe miezi sita bila kumpa mtoto kitu kingine. **PICHA: MTANDAO**

Inaelezwa kuwa wanawake wengi hasa wa mjini na majijini wanakataa kunyonyesha watoto wao vema kwa kuhofia kuharibika maumbo baada ya kunenepa zaidi, maziwa kusinyaa na kulala.

Kwa vijijini wanaacha kunyonyesha na kukimbilia kwenye kazi za kuzalisha chakula na kupata muda mchache wa kunyonyesha, hali inayoamsha sauti za wadau.

Khadija Nasibu, ni Ofisalishe Halmashauri ya Ushetu, mkoani Shinyanga, anayesema, moja ya sababu zinazorudisha nyuma jitahada za kunyonyesha maziwa ya mama ni imani potofu ya kuwa maziwa ya kwanza yanapaswa kutupwa. Maana ni machafu.

Sababu nyingine ni imani kuwa maziwa pekee hayawezi kumtosha mtoto anapozaliwa hadi miezi sita, wengine wanasema mtoto analia sana hashibi bila kutafuta chanzo cha kilio.

Kuna baadhi wanadai kuwa kuwapatia watoto wachanga maji mara baada ya kuzaliwa ni muhimu na lazima, yote hayo yakichangia kukiuka maelekezo na sera ya kuwanyonyesha miezi sita bila kulishwa chochote.

Anasema, wapo wanawake wanaoamini kuwa maziwa yao yanasababisha watoto kuwa na kiu, wengine wanadai wakinyonyesha vile inavyotakiwa matiti yao husinyaa, kuanguka na kupoteza mvuto na baadhi wanadai mtoto anaponyonya anahitaji maji ya nyongeza hasa wakati wa joto.

**UNYONYESHAJI UNAOFAA**

Khadija anasema, inashauriwa mama anapoojifungua apewe mtoto amshike akiwa hajavaa nguo na kumweka juu ya mwili wake ili ngozi ya mama na mtoto zigusane na aanze kunyonyeshwa ndani ya saa moja baada ya kujifungua ili mtoto amtambue mama kwa harufu yake.

Anasema, mtoto anahitaji kunyonyeshwa kwa muda wa dakika 15 hadi 20 katika titi moja na kila baada ya saa mbili kwa kipindi cha miaka miwili bila kumuachisha ziwa, tena kufanya hivyo kutakomaza ubongo atakuwa mwepesi wa kutambua vitu hasa vile vitakavyokuwa vinamzunguka kwenye makuzi.

"Endapo mama ana maambukizi ya VVU, aanze dawa au kuendelea kuzitumia huku akimnyonyesha mtoto maziwa pekee kwa miezi sita, halafu amwanzishie vyakula vya nyongeza na kuendelea kumnyonyesha hadi atakapotimiza miaka miwili au zaidi,"anaongeza Khadija.

Aidha, mama anayefanya kazi mbali anaweza kuendelea kumnyonyesha mtoto mara kwa mara hasa pale anapokuwa naye au kukamua maziwa na kuyahifadhi mahali safi na salama ili mlezi amnyonyeshe, mama akiwa kazini.

**KILIMO NI KIKWAZO**

Kaimu Mganga Mkuu wa Hospitali ya Ushetu Dk. Jenviva Gabriel anasema, wengi wa wazazi wanaacha kuwanyonyesha watoto na kukimbilia shambani kulima wakati mtoto anahitaji maziwa ya mama.

Anasema maziwa hayo ni muhimu kukomaza ubongo, kukua ipasavyo na kukingwa na magonjwa ya binadamu akiwashauri kuzingatia unyonyeshaji kama ambavyo wamekuwa wakikumbushwa kliniki.

Anasema, mtoto asiyenyonyeshwa ipasavyo anakosa uwezo wa kutunza kumbukumbu na kile anachofundishwa shuleni au watu wanaomzunguka hakitakaa akilini na mwisho atashindwa kufanya vema kwenye masomo na shughuli za kijamii.

Dk. Jenviva anasema, kila mjamzito au mama mwenye wa-

**Inaendelea Uk. 12**

AFYA

# Vita dhidi ya kuzalisha, matumizi, biashara ya dawa za kulevya, serikali kukomalia sera

**NA SABATO KASIKA**

VITA dhidi ya dawa za kulevya, inapoendelea kupamba moto, ripoti zinaonyesha kwamba kiasi kikubwa cha dawa hizo kinachofikia kilo 1,965.34 kilikamatwa mwaka jana.

Kiwango hicho kinaelezwa na serikali kuwa ni karibu mara saba zaidi ya kiasi kilichowahi kukamatwa tangu Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya (DCEA) ilipoanzishwa miaka saba iliyopita.

Kutokana na hali hiyo, serikali inatangaza kuongeza kasi ya kusimamia Sera ya Taifa ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya ya mwaka 2024, ikieleza kuwa matokeo ya juhudi hizo yameanza kuonekana.

Hayo yamo katika taarifa ya hivi karibuni ya Ofisi ya Waziri Mkuu (Sera, Bunge na Uratibu) inayoofafanua kuwa sera hiyo inaitaka serikali kushirikiana na wadau mbalimbali kuimarisha huduma za tiba kwa waraibu wa dawa za kulevya.

Pia , kuratibu na kupanua huduma za upataji nafuu kwa watumiaji wa dawa za kulevya na kuendelea kutoa elimu kwa umma kuhusu madhara ya dawa za kulevya kupitia njia mbalimbali.

Wizara inataja njia hizo kuwa ni kupitia vyombo vya habari, matukio ya kitaifa, semina, makongamano, mitandao ya kijamii na vipeperushi na kwamba mkakati huo ni muhimu kupunguza matumizi haramu ya dawa za kulevya kwa makundi rika tofauti kulingana na mahitaji.



Dawa za kulevya zinazotishia hatima ya vijana wakubwa kwa wadogo. **PICHA: MTANDAO**

"Kwa kuzingatia sera hiyo, serikali itaendelea kushirikiana na mataifa mengine na taasisi za kimataifa katika kukabiliana na tatizo la dawa za kulevya. Kushirikiana na taasisi za kimataifa, ni kubadilishana uzoefu, kushiriki mafunzo na kupanga mikakati ya pamoja ya namna ya kukabiliana na tatizo la dawa za kulevya," inasema Ofisi ya Waziri Mkuu.

Aidha, katika taarifa ya hali ya dawa za kulevya ya mwaka 2023, serikali inashirikisha asasi za kiraia 63 kutoa elimu kwa makundi ya kijamii na kufanikiwa kunasa kiasi hicho cha tani 1,965.34 za dawa.

Kamishna Jenerali Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya (DCEA), Aretas Lyimo, anasema taarifa hiyo ni ya muhimu ili jamii ijue na ishiriki katika vita dhidi ya dawa za kulevya inafanyika.

"Tatizo la dawa za kulevya ni mtambuka linahitaji ushirikishwaji wa wadau, hivyo ni muhimu kushirikiana ili kuikomesha, kwani taarifa yetu inajumuisha shughuli mbalimbali zilizofanywa na wadau wa udhibiti wa dawa za kulevya wa ndani na nje ya nchi," anasema Lyimo.

Lyimo anasema, katika miaka saba tangu DCEA ianzishwe, imepanua wigo wa udhibiti wa dawa za kulevya kwa kufungua ofisi katika mikoa ya Arusha, Mbeya, Mtwara, Mwanza na Dodoma.

MAONI YA WADAU

Mkurugenzi wa shirika la kiraia linalohudumia waraibu wa dawa hizo la Life and Hope Rehabilitation Organisation (LHRO), Al-karim Bhanji, anazungumzia taarifa hiyo ya serikali akisema wameanzisha huduma za kuhudumia waraibu.

Anasema wanatoa elimu ya kuwajengea uwezo waraibu kutambua haki zao za msingi, kata tano wilayani Bagamoyo mkoani Pwani.

Anazitaja kata hizo kuwa ni Dunda, Nianjema, Magomeni, Kisutu na Kiromo, huku akifafanua kuwa wanafanya kazi hiyo kwa wahisani mbalimbali wa ndani na nje ya nchi.

"Vilevile, tunawashukuru wadau wengine vikiwamo Vituo vya Kudhibiti na Kuzuia Magonjwa CDC, Wadau wa Huduma za Waraibu (MAT) na Shirika la Tanzania Health Support (THPS), kwa jinsi ambavyo nao wamekuwa nasi bega kwa bega katika kazi hii," anasema.

Bhanji anasema, wanashirikisha wadau mbalimbali, wakiwamo waraibu, wauguzi, viongozi wa dini, polisi, madaktari, wataalam wa sheria, walimu, wanafunzi, maofisa ustawi wa jamii na makundi mengine ndani ya jamii, katika utoaji wa elimu hiyo, ili kila mmoja ajue wajibu wake.

"LHRO inachokifanya Bagamoyo, ni kutekeleza Sera ya Taifa ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya ya mwaka 2024 ambayo ni kuelimisha umma kuhusu madhara ya dawa hizo," anasema.

Anasema shirika lake limejikita upande wa pili katika utoaji wa elimu, kwa kuwaelimisha waraibu kujua haki zao za msingi ili kupunguza unyanyapaa wanaokumbana nao ndani ya familia na katika jamii.

# Imani hizi potofu zinavyowanyima watoto haki ya kunyonya, wakianzishiwa vyakula mapema

**Inatoka Uk. 11**

wale wenye watoto wanaohitaji lishe waandae vyakula vyenye lishe bora na sio kula alimradi ili kukabili utapiamlo na udumavu.

Anasema, moja ya faidi ya unyonyeshaji huo ni kuwakinga watoto dhidi ya magonjwa hatari, kujenga mahusiano ya hisia baina ya mtoto na mama, kuchangia afya na maisha bora ya mama kwani humpunguzia hatari ya kupata saratani ya mfuko wa mayai ya uzazi na matiti.

Jenviva anasema, ili kuondoa tatizo hilo wahudumu wa afya watawafikia wajawazito kipindi cha kliniki kinachokutanisha wazazi na watoto wanaopata huduma kuwaelimisha umuhimu wa kunyonyesha.

Anasema watakuwa pamoja watoa huduma ngazi za jamii ambao wengi wao wanaishi na kinamama hao mitaani au vijijini.

Anasema, wastani wa watoto wanne hadi watano kati ya 10 ndio hunyonyeshwa kwa miezi sita pekee ya mwanzo, sehemu kubwa ya watoto hao hupewa maji wakiwa na miezi miwili na wengine kuanzishiwa maziwa na kuachishwa kunyonyeshwa jambo ambalo ni hatari kiafya.

Anasema elimu ya unyonyeshaji ambayo watakuwa wanaitoa siku za kliniki itakwenda pamoja na makundi ya aina ya vyakula vyenye lishe bora kwa watoto na wajawazito ili kutambua namna sahihi ya kuandaa vyakula hivyo na kuwataka wajawazito na wenye watoto wadogo kuhudhuria kliniki vipindi vyote.

**USHUHUDA WA WAZAZI**

"Utandawazi umewafanya wasichana na kinamama wengi kuona kunyonyesha ni adhabu inayoharibu miili au shepu zao. Asilimia kubwa wanaofanya hivyo ni wale wenye umri wa kuanzia miaka 20 mpaka 30." Anasema mkazi wa kata ya Uyogo, Amina Musa (52).

Anakumbusha kuwa miaka ya nyuma walikuwa wakinyonyesha watoto mpaka miaka miwili na elimu ya uzazi vijijini haikuwepo na wakati mwingine walilazimika kuwaachisha watoto kwa nguvu kwa kupaka vitu mbalimbali kwenye matiti, na watoto wao walikuwa na afya na nguvu ikilinganishwa na watoto wa zama hizi ambao wengi afya zao zimelegalega.

"Anaungwa mkono na Angelina Mabula (60) kutoka Segese-Msalala anayesema, aliolewa akiwa na umri mdogo na alifundishwa na bibi yake kuwa mtoto mchanga ananyonya maziwa ya mama miaka miwili na anatakiwa kunyonya miezi sita ya mwazo bila chakula chochote na alizingatia maelekezo hayo.

Anasema, kuna wakati alikuwa akiadhibiwa na bibi yake kwa kutokumnyonyesha mtoto kwa wakati hata akiwa shambani alikuwa akipata muda wa kunyonyesha tofauti na sasa wazazi wengi wakimaliza miezi sita ya kwanza na kurejea kazini wanawaachia watoto dada wa kazi.

**ATAJA MADHARA**

Mkazi wa mtaa na kata ya Nyasubi Manispaa ya Kahama ambaye hakutaka jina lake kuandikwa, anasema kutonyonyesha watoto ipasavyo kwa kipindi cha miaka miwili na kusababisha wapate changamoto, ikiwamo kudhohofika na kushindwa kumudu masomo.

Anasema baada ya kujifungua mwaka 2007 hakunyonyesha vema miezi sita ya mwanzo kwani alipopata nguvu alimwachia mfanyakazi naye akaenda kazini alikuwa ameajiriwa katika nyumba za kulala wageni.

Anasema, mtoto huyo alikuwa dhaifu na alipofikisha umri wa kwenda shuleni hakuweza kusoma kwasababu hawezi kushika peni wala penseli.

Anaendelea kusimulia, mtoto wa pili alijitahidi kufuata ushauri wa madaktari na wauguzi wa kunyonyesha vema miezi sita ya mwanzo mpaka miaka mwili, aliona mabadiliko ya ukuaji wa mtoto huyo ana nguvu na anaendelea na masomo vema.

AFYA

# Shirika na mchakamchaka wa elimu ya uzazi kwa vijana

**Na Beatrice Philemon**

HAKI ya afya ya uzazi si jambo la upendeleo ni stahili ya kila mmoja hasa vijana ambao wanatakiwa kupata elimu, taarifa, maarifa na huduma bila kizuizi.

Hata hivyo, kuna taarifa kuwa vijana wengi hawafahamu kuwa wana haki hiyo na ile ya kushiriki kwenye ngazi mbalimbali za uamuzi ili kutoa changamoto zinazowakabili hatimaye serikali iwasikilize na kuwapa mahitaji wanayostahili.

Cuthbert Maendaenda ni Mkurugenzi wa Shirika la Tanzania Men as Equal Partners in Development (TMEPiD), anasema wamebaini kuwa vijana wengi hawaifahamu haki hiyo ya kupata huduma za uzazi.

Katika kuwafikia anaeleza kuwa TMEPiD imekuja na mpango maalumu wa kuwaelimisha, kuhusu afya ya uzazi na jinsi ya kushiriki kwenye ngazi mbalimbali za maamuzi popote walipo ili kuwasilisha changamoto zinazowakabili ambazo ni pamoja na masuala ya afya ya uzazi.

Anasema lengo la mafunzo wanayotoa ni kuwasaidia vijana kusambaza elimu ya afya ya uzazi kwa wenzao, kujua haki zao, kushiriki kwenye vyombo vya maamuzi hasa kwenye kamati za vituo vinavyotoa huduma za afya ili kujadili masuala hayo na kuibua changamoto zao.

"Pia tunawasaidia kushiriki na kufuatilia vikao vya maendeleo ngazi ya wilaya na kujua jinsi ya kutetea haki zao." Anasema Maendaenda.

Anaongeza kuwa, hadi sasa wametoa mafunzo mkoa wa Dodoma, Shinyanga, Mara, Pemba na Unguja, Simiyu na Dar es Salaam kupitia programu ya 'Safeguard Young People (SYP) kwa ufadhili wa Shirika la Umoja wa Mataifa la Idadi ya Watu (UNFPA).

"Wakati wa mafunzo tuwamefundisha vijana kutetea haki zao kupitia mfumo wa 'Smart- Advocacy' au utetezi makini, kushiriki na kufuatilia vikao vya maendeleo ngazi ya wilaya na kushiriki kwenye kamati za vituo vinavyotoa huduma za afya." Anaongeza Mkurugenzi

**MAFANIKIO YA MAFUNZO**

Kutokana na elimu waliyoipata kwa TMEPiD, hivi sasa vijana wengi waliofikiwa wana uwakilishi wa aina mbalimbali kwenye ngazi za maamuzi, anasema Maendaenda.

Aidha, kumekuwa na ushiriki wa wanaume kwenye huduma za afya ya uzazi, hivi sasa wanaume wanakwenda kwenye vituo vya afya kupata elimu na huduma za uzazi wa mpango sambamba na wenza wao tofauti na miaka ya nyuma.

Mbali na hilo, anasema kwamba wanashiriki kwenye hamasa kama kiini cha mabadiliko kwa wanaume wenzao mitaani na popote walipo, anasema na kuongeza kuwa miaka ya nyuma, wanaume walikuwa waoga kupima VVU kwenye kliniki au vituo vy CTC, lakini kupitia elimu hiyo kumekuwa na ongezeko la wanaume wanaopima hali zao pamoja na wenza.



Kukosekana elimu ya uzazi na jinsi ya kujizuia na mihemko ya kujamiiana kunasababisha vijana kujiingiza kwenye uhusiano wenye changamoto. **PICHA: MTANDAO**

Mbali na hilo, TMEPiD iliratibu kusainiwa kwa makubaliano kati ya Tanzania na Shirika la Umoja wa Mataifa la Idadi ya Watu (UNFPA), kuhusu kuchangia pesa za kununua vifaa vya tiba na kwa miaka mitano ambapo kila mwaka UNFPA itatoa Dola za Marekani milioni 2.6 na serikali itakuwa inachangia asilimia moja na kadri miaka inavyoendelea itaongeza.



Anasema mafunzo haya yametolewa kwa lengo la kutimiza matakwa ya kimataifa ya kuzifanya huduma ya afya uzazi wa mpango kuwa ni haki ya kila mtu bila kujali jinsi yake, hali ya ndoa ili kuwawezeshawanawake kufanya maamuzi wenyewe kuhusu mahitaji ya uzazi wa mpango.

Maendaenda anaongeza kuwa, pia wanataka vijana wapewe haki ya kupata elimu na huduma ya uzazi wa mpango bila kujali wapo shule au popote.

"Pia haki ya usawa wa kijinsia iingizwe kwenye uzazi wa mpango pamoja na VVU na UKIMWI na tiba ya magonjwa yatokanayo na kujamiana STIs".

**SAUTI ZA WANUFAIKA**

Sabina Lister (25), anayeishi Kigamboni Dar es Salaam ni miongoni mwa vijana 78, waliopata mafunzo yanayotolewa na TMEPID kwa kushirikiana na UNFPA.

"Wakati wa mafunzo tulifunzwa afya ya uzazi, faida zake, jinsi ya kutafuta changamoto ambazo zipo kwenye jamii, uzazi wa mpango, UKIMWI, ndoa za utotoni, dawa za kulevya, jinsi ya kupata mikopo kutoka kwenye taasisi za kifedha, namna ya kuunda vikundi ambavyo vitatoa elimu ya afya ya uzazi kwa vijana wenzetu na kuzuia mimba za utotoni" anasema.

Sabina anaeleza kuwa, mafunzo yameleta mabadiliko makubwa kwa vijana katika manispaa hiyo na hivi sasa vijana wanapata nafasi ya kushiriki kwenye ngazi za maamuzi hasa kwenye kamati za vituo vinavyotoa huduma za afya na kuwakilisha mahitaji yao yanayohusu haki ya afya ya uzazi tofauti na miaka mingine.

Anasema kupitia elimu waliyoipata kutoka TMEPiD, wameunda kikundi cha vijana chenye wanachama nane ili kutoa elimu kuhusu afya ya uzazi kwa vijana wenzao Kigamboni, hivi sasa wana uwezo wa kushiriki kwenye ngazi za maamuzi na kutoa hoja zao.

"Hivi sasa tumeanza kutoa elimu ya afya ya uzazi kwa vijana wenzetu kwenye hospitali kwa kushirikiana na Mganga Mkuu wa Hospitali,' anasema

Pia, wanatumia kikundi chao kujadili masuala ya afya, changamato zinazowakabili katika jamii yao na jinsi ya kudai haki zao.

Anawashukuru TMEPiD na UNFPA kwa kuanzisha mafunzo haya kwa sababu elimu hii imewafungua macho vijana, hivi sasa idadi ya wanaokwenda kwenye vituo vya afya kupata taarifa kuhusu haki ya afya ya uzazi anaongeza.

Anawaomba wadau ikiwamo TMEPiD waendelee kutoa elimu hii katika maeneo mengine kwa sababu vijana wengi kutoka mikoani hawafahamu elimu hiyo ambayo inasaidia kupambana na magonjwa ya kuambukiza, mimba za utotoni, VVU na UKIMWI," anasema.

AFYA

# Inaelezwa ni raha kujifungulia ndani ya maji ya jakuzi

**Na Moshi Lusonzo**



Mama akiwa kwenye jakuzi akisubiri kujifungua. **PICHA: MTANDAO**

KUNA baadhi ya wanawake wanaogopa kubeba ujauzito wakihofia hekaheka zinazoambatana na maumivu makali wakati wa kujifungua.

Hata hivyo, kuna wengine wanaomba kuzalishwa kwa upasuaji kwa kuogopa misukosuko ya kujifungua kwa njia ya kawaida.

Jambo zuri linaloleta faraja kwa sasa ni kuanzishwa kwa huduma ya kujifungulia ndani ya maji, ambayo inatoa ahuweni wale wanaogopa maumivu.

Hospitali ya Taifa ya Muhimbili, hivi karibuni imezindua huduma hiyo ambayo inaelezwa ni salama kwa mama na mtoto.

Mkurugenzi wa Hospitali hiyo, Profesa Mohamed Janabi, anasema kujifungua kwa njia hiyo kumeanza kutumika miaka mingi Marekani, Ulaya na Afrika Magharibi, lakini Muhimbili ni huduma mpya inayoanza sasa.

Anasema mama wajawazito wataingizwa kwenye jakuzi lenye maji ya moto kujifungua.

"Maji ya moto yaliyowekwa kwenye jakuzi yanamfanya kuwa na hali ya kawaida, mzunguko wa damu kuwa wa kawaida na kupunguza maumivu wakati wa kujifungua,"

### FAIDA ZA JAKUZI

Kwa mujibu wa Profesa Janabi, zipo faida nyingi kwa mama kujifungua ndani ya maji akitaja mojawapo kuwa ni kutuliza maumivu na pia huchukua muda mfupi.

Anasema nyingine ni kudhibiti mishipa ya mfuko wa kizazi kujikaza na kusababisha kuchanika wakati wa kujifungua, tena inapunguza shinikizo la damu, kuondoa wasiwasi na kuongezeka vichocheo (homoni) zinazosababisha mama kufadhaika.

Mtandao wa Medicover, unaeleza kwamba kujifungua ndani ya maji kuna manufaa kwa mtoto mchanga, kwani hupunguza mshutuko wakati akiingia duniani.

Unaeleza kwamba maji ya moto yaliyowekwa katika jakuzi yanafanana na yale ya mfuko wa uzazi kwenye tumbo la mama

Mtoto ambaye ana miezi tisa tumboni wakati akijiandaa kutoka, hupata urahisi wa kuingia duniani kupitia njia hiyo, pia humpunguzia mama msongo wa mawazo kiasi unaosababishwa na uchungu.

Kihistoria njia hiyo ya kufungua ni ya kale, inahusishwa na imani na hadithi mbalimbali za enzi hizo. Nyingi zinaelezea namna njia hiyo ilivyo salama kwa ujio wa mtoto duniani

Hata hivyo, ni lazima ieleweke kwamba kujifungua ndani ya maji ni sehemu ya kupunguza hatari hasa kwa ujauzito wenye hatari.



Mtandao wa Medicover, unasema wanawake wenye historia ya shinikizo la damu, kufanyiwa upasuaji, kisukari, kujifungua kabla ya wakati na hata mtoto mwenye uzito dogo, wanashauriwa kufuatiliwa kwa ukaribu kabla ya kuruhusiwa kuingia majini.

"Zaidi ya hayo, kujifungua ndani ya maji si chaguo zuri ikiwa mama ana matatizo kama vile mfuko wa uzazi kuongezeka upande wa mlango wa kutokea mtoto na kuziba njia ya uzazi.

### MWONGOZO UNAOTUMIKA

Kwa mujibu wa mapendekezo ya kitaalamu, wanawake wanaochagua kuzaa kwenye maji wana uwezekano mkubwa wa kuzaa kawaida, hivyo mjamzito anapaswa kuchagua.

Wajawazito wanatakiwa kutafuta ushauri wa matibabu kila wakati katika umri wote wa kubeba mimba na kujifungua na kwamba ni muhimu kufuata mapendekezo ya daktari na kuchukua hatua zinazofaa kiusalama.

Mkunga Agnes Ndunguru, kutoka hospitali moja mjini Songea mkoani Ruvuma, akizungumza na BBC, anasema amewasaidia wajawazito kujifungua kwa njia hiyo ya jakuzi.

Anafafanua kuwa kujifungua kwa aina hii humpunguzia mama maumivu lakini pia, huzuia kuchanika njia wakati wa kujifungua.

" Maji yanaondoa uwezekano wa njia ya uzazi na sehemu za siri za mama kuchanika lakini pia mkao wa mama kwenye jakuzi humwezesha mtoto kutoka bila hatari.' Anaeleza Agnes.

Anaongeza kuwa uzazi huo unaweza kufanyika nyumbani au hospitali kutegemea na sera na miongozi ya nchi na kwa Tanzania huduma hii inapatikana hospitalini.

### INSTAGRAM

"Wanasayansi walifanya utafiti wakaona ni njia yenye mafanikio, inampa utulivu na amani mama, maana kuna kichocheo (homoni) cha kusaidia maendeleo ya kujifungua yawe vizuri kinapanda hivyo hufanya njia ifunguke kwa urahisi na mtoto kuzaliwa bila matatizo", anaongeza Agnes.

Anaeleza kuwa wanawake wengine huchagua kuingia kwenye maji wakiwa katika hatua za awali kisha hutoka na kujifungulia nje ya jakuzi.

Akinukuu wataalamu anasema njia hiyo ni salama na mtoto anapozaliwa kwenye maji anakabiliwa na hatari ndogo ya kupata matatizo ya kupumua ikilinganishwa na anayezaliwa nje ya maji.

Kwa kuwa mtoto anaishi kwenye maji katika mji wa mimba, hivyo anapozaliwa ndani ya maji hawezi kuhangaika kutafuta hewa ya nje.

Agnes anatambulishwa hospitali mbalimbali ikiwa ni mwaka wake wa pili, akisema amepata mwitikio mkubwa kwasababu wataalamu wengi wanapitia tafiti mbalimbali kuhusu huduma hii.

Ni ndoto ya mkunga huyu kuhakikisha kuwa huduma ya kujifungua ndani ya maji inasambaa Tanzania nzima kwa lengo la kupunguza vifo vya watoto wachanga na wazazi.

### SHUHUDA YA UZAZI

"Sikuamini kama inawezekana kujifungua ndani ya maji," anasema Eliminata Fabian, mkazi wa Dar es Salaam, aliyejifungua mapacha.

Anajifungua watoto hao kwenye maji, njia ambayo imekuwa ikipata umaarufu nchini ikianzia Hospitali ya Taifa Muhimbili.

Eliminata aligundua huduma hii kupitia mitandao ya kijamii, akitaja ukurasa wa Instagram wa mkunga Agnes.

"Nilivutiwa pale nilipoona watu wanajifungua kwa njia hii nilijaribu kuulizia nikaambiwa kuna nafuu sana, maumivu yanapungua tofauti na njia ya kawaida." Anasema.

Anaongeza: "Siku ya kujifungua sikuamini, kama ujuavyo maumivu kwa kawaida ni makali, lakini kulikuwa na tofauti maumivu ya ndani ya maji na ya njia ya kawaida ni tofauti mno."

Anaeleza kuwa kujifungua mapacha kwenye jakuzi kumemjengea kujiamini na anatamani kuendelea na njia hii kwa uzao ujao.

Kazi kubwa ya watoa huduma hii ni hamasa kwa umma kwa kuwa mara nyingi jamii haiamini kuwepo kwa uzazi ndani ya jakuzi.

"Kwa kuwa huduma hii ni mpya hapa nchini kuna maswali mengi kama vile mtoto akiingia kwenye maji hawezi kuyanywa ? Mtoto hatakufa? Hataambukizwa maradhi "

Hospitali ya Taifa ya Muhimbili inapokea wateja wanaochagua kujifungua kwa upasuaji kuepuka maumivu au sindano ya ganzi hivyo serikali imeruhusu njia hiyo kutumiwa, anasema Agnes na kuwataka kinamama kuitumia.



# Wadaiwa kulipana posho fedha za uhamasishaji lishe bora kwa watoto

**Na Thobias Mwanakatwe,**
SINGIDA

BAADHI ya wataalam wanadaiwa kuchangia udumavu wa watoto katika mikoa ya Kanda ya Kati kufikia asilimia 28.9 kutokana na kiwango kikubwa cha fedha zinazotengwa na Serikali kuhamasisha lishe bora kudaiwa kulipana posho badala ya kutatua changamoto hiyo katika jamii.

Katibu Tawala Mkoa wa Singida, Dk. Fatuma Mganga alitoa madai hayo juzi wakati akifungua semina ya utoaji matokeo ya utafiti wa afya ya uzazi na mtoto na viashiria vya ugonjwa wa malaria kwa kanda hiyo uliofanywa na Ofisi ya Taifa ya Takwimu nchini.

Semina hiyo imewashirikisha maofisa mipango, wauguzi, waratibu wa malaria, mameneja takwimu, maofisa lishe, waganga wakuu wa wilaya na waratibu wa huduma za mama na mtoto wa mikoa ya kanda hiyo ya Dodoma, Singida na Manyara.

"Matokeo yanaonesha hali ya udumavu bado ni kubwa asilimia 28.9, takwimu hii ni karibu sawa na wastani wa kitaifa ambao ni asilimia 30, hali hii imesababisha kuendelea kuwepo kwa vifo vya watoto chini ya miaka mitano," alisema.

Dk. Mganga alisema Manyara inaongoza kwa kuwa na kiwango kikubwa cha udumavu ambacho ni asilimia 32, ukifuatiwa na Dodoma 30.7 na Singida 25.7.

Alisema inashangaza kuona mikoa hiyo katika kutenga fedha kwa ajili ya lishe inafanya vizuri, lakini inakuwa vinara wa tatizo la udumavu hali ambayo inaonesha fedha hizo haziakisi uhalisia unaotakiwa.

"Yawezekana unapanga fedha za lishe, lakini mwanzo mwisho umepanga ya kikao, hela ya kusaidia watoto tunajisaidia sisi wenyewe, masuala ya posho tugawane kwenye vyanzo vingine, za lishe tuache ili angalau tusaidie masuala ya lishe," alisema.

Dk. Mganga, alisema kimsingi tatizo la udumavu katika mikoa hiyo halisababishwi na wazazi bali watalaam kwa kushindwa kuwajibika katika majukumu waliyopewa.

Alisema wakati umefika wa kubadilika ili kuondokana na tatizo la udumavu kwenye mikoa hiyo.

Alisema maofisa mipango na lishe waoneshe uzalendo katika kupunguza udumavu kwa watoto kwa kuhakikisha fedha zinazotengwa zinalekezwa kukabiliana na tatizo hilo na sio kulipana posho.

Mtakwimu Mwandamizi kutoka Ofisi ya Taifa ya Takwimu Dodoma, Prisca Mkongwe, alisema katika utafiti uliofanyika 2021/2022, hali ya udumavu kitaifa ni asilimia 30 na vifo vya wajawazito vimepungua kutoka 503 na kufikia 104 katika kila vizazi hai 100,000.

Alisema katika kipindi cha 2015/2016, asilimia 63 ya watoto walikuwa wanakufa kabla ya kufikisha miaka mitano, lakini kwa sasa kiwango hicho kimepungua na kufikia asilimia 43 katika kila vizazi hai hivyo.

Ofisa Lishe wa Mkoa wa Singida, Teda Sinde, alisema kiwango cha udumavu katika mkoa huo kimepungua kutoka asilimia 29 na kufikia asilimia 25 kutokana na jitihada zinazofanyika kutoa elimu kwa jamii kuhusu lishe.

Sinde, alisema changamoto ya udumavu inasababishwa na ulishaji na unyonyeshaji watoto wadogo, hivyo mkoa umejipanga kuanzisha mapishi darasa katika vijiji ili kuwapa elimu ya lishe wananchi.

## Mpango ataka vibali ukataji miti vipunguzwe

**Na Paul Mabeja,**
CHAMWINO

MAKAMU wa Rais, Dk. Philp Mpango ameutaka Wakala wa Huduma za Misitu Tanzania (TFS) Mkoa wa Dodoma kupunguza utoaji vibali vya kukata miti kwa ajili ya kuchoma mkaa ili kubidhibiti kukithiri kwa uharibifu wa mazingira.

Dk. Mpango alitoa rai hiyo juzi wilayani hapa wakati wa ziara yake ya siku tatu mkoani Dodoma ya kukagua miradi ya maendeleo.

Alisema elimu inapaswa kutolewa kwa wananchi ili waweze kutumia nishati safi ambayo ni mbadala kwa ajili ya kupikia na kusisitiza utunzaji wa mazingira kwa kupanda miti kwa wingi ili kupunguza changamoto ya mabadiliko ya tabia nchini.

Naibu Waziri wa Maliasili na Utalii Dustan Kitandula, alisema Wizara yake itaendelea kusimamia na kulinda maliasili zilizopo nchini na wananchi wanaokabiliwa na changamoto ya wanyama wakali na waharibifu.

Kitandula aliongeza kuwa wizara hiyo itaendelea kupambana na changamoto ya mabadiliko ya tabianchi kwa kuhimiza utunzaji wa misitu na upandaji wa miti maeneo yaliyoathirika kwa uharibifu wa mazingira.



Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, Justin Nyamoga (kushoto), akipitia taarifa ya utendaji ya Halmashauri ya Wilaya ya Musoma mkoani Mara, walipokutana Bungeni, jijini Dodoma jana. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

# Waziri Biteko aimwagia sifa EWURA

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

NAIBU Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati, Dk. Doto Biteko ameipongeza Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA) kwa kuandaa Mwongozo wa Usimamizi wa Usafi wa Mazingira na Topekinyesi ili kukabiliana na uchafuzi wa mazingira nchini.

Pongezi hizo zilitolewa juzi kwenye hotuba yake iliyosomwa katika Kongamano la Kitaifa la Usafi wa Mazingira kwa niaba yake na Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu (Sera, Bunge na Uratibu), William Lukuvi.

"Naipongeza EWURA kwa kuja na mwongozo huu wa Kiswahili ambao unalenga kuziongoza mamlaka za majisafi na usafi wa mazingira kutoa huduma ya usimamizi wa tope kinyesi kwa wananchi walio nje ya mtandao wa majitaka," alisema

Biteko, aliipongeza EWURA kwa kuboresha mfumo wa uwasilishaji taarifa za mamlaka hizo ambao utatoa fursa ya kupata takwimu sahihi kuhusu usafi wa mazingira kusaidia mipango ya maendeleo katika sekta ya maji, afya na mazingira.

Alisema mwongozo huo unawalenga wadau kama mamlaka za serikali za mitaa, sekta binafsi za kutoa huduma ya usafi wa mazingira kwenye maeneo yasiyo na mtandao wa majitaka, wizara zenye dhamana, RUWASA na NEMC.

Alisema taarifa ya EWURA ya utendaji wa mamlaka hizo kwa mwaka 2022/23, inaonesha 21 kati ya 85 sawa na asilimia 24.7 ndizo zenye miundombinu ya kutibu majitaka na tope hilo kwa kipindi hicho.

Aidha, taarifa za Wizara ya Maji zinaonesha hadi Aprili, 2024 mtandao wa majitaka nchini ulikuwa kilometa 1455.93 ikilingalishwa na kilometa 1416.9 za Aprili, 2023.

Alisema idadi ya maunganisho katika mtandao, usafirishaji na kutibu majitaka umefikia kilometa 58,650 kutoka 56, 923 kwa kipindi kama hicho kwa mwaka jana..

Waziri wa Maji, Jumaa Aweso aliipongeza EWURA kwa kuwakutanisha wadau kujadili kuimarisha usimamizi wa mazingira.

Awesu, alisema kuzinduliwa kwa mwongozo huo kutasaidia mamlaka za maji na wadau katika usimamizi wa huduma za usafi wa mazingira na tope hilo la kinyesi kuongeza ufanisi zaidi

Alizikumbusha mamlaka za maji nchini kuzingatia mwongozo huo kwa misingi, mipaka, wajibu na majukumu ya utoaji huduma za usimamizi wa tope hilo zinazofanywa na mamlaka hizo.

Mkurugenzi Mkuu wa EWURA, Dk. James Andilile, alisema tathmini na tafiti zilizofanywa kutoka karne ya 19 zilibainisha watu wanapokaa kwenye mazingira safi, afya zinakuwa imara na ni njia ya kujikinga na magonjwa ya milipuko.

Makamu Mwenyekiti wa Bodi ya EWURA, Victoria Elangwa, alisema katika kongamano hilo kutakuwa na mawasilisho yatakayosaidia wataalam kuchakata namna bora ya kutunza mazingira na kuahidi bodi hiyo kusimamia..



# TRA: Hatutawadai risiti wafanyabiashara wa mbao

**Na Elizabeth John,**
NJOMBE

MAMLAKA ya Mapato Tanzania (TRA) Mkoa wa Njombe imesema katika mwaka wa fedha wa 2024/2025 haitawadai wafanyabiashara wa mbao risiti za manunuzi ya mbao kutoka kwa mkulima.

Imesema bali wafanyabiashara hao wanatakiwa kuwa na barua ya uthibitisho wa mauziano ya mbao kutoka kwa watendaji wa vijiji husika.

Hayo yalielezwa na Ofisa Elimu na Mawasiliano TRA Njombe, Brain shoo, wakati akizungumza na waandishi wa habari kuhusiana na mabadiliko ya sheria za kodi katika mwaka wa fedha wa 2024/2025.

Shoo alisema mamlaka hiyo haitadai risiti ya manunuzi ya mbao kwa kuwa mkulima siyo mfanyabiashara na hana mashine ya kielektroniki.

"Kuna baadhi ya wafanyabiashara wamekuwa wakilalamika kwamba wakienda kufanya manunuzi ya mbao kutoka kwa mkulima ambaye sio mfanyabiashara tunawadai risiti ya manunuzi, naomba niseme kwamba sisi hatutuwadai risiti ya manunuzi," alisema Shoo.

Alisema wafanyabiashara wanaonunua mbao kutoka kwa mkulima wanatakiwa kuwa na barua ya uthibitisho kutoka kwa Mtendaji wa Kijiji husika, huku wale wanaonunua shamba la miti ndipo wavune mbao wakitakiwa kuwa na mkataba wa mauziano ya shamba hilo.

**Hayo yalielezwa na Ofisa Elimu na Mawasiliano TRA Njombe, Brain shoo, wakati akizungumza na waandishi wa habari kuhusiana na mabadiliko ya sheria za kodi katika mwaka wa fedha wa 2024/2025.**

Aidha, aliwataka wafanyabiashara wenye mtaji wa kuanzia Sh.milioni 11 kuwa na mashine za kutolea risiti za kielektroniki, huku akiwakumbusha wananchi kudai risiti pindi wanaponunua bidhaa mbalimbali ili serikali ipate kodi stahiki.

Mwenyekiti wa Jumuiya ya Wafanyabiashara Mkoa wa Njombe na Nyanda za Juu Kusini, Sipahely Msigala, alisema mfumo uliowekwa na TRA wa kuwataka wakulima mbao wawe na risiti za EFD ulisababisha adha kwa wafanyabiashara.

Alisema: "Bado kuna haja ya TRA kuondoa hata hiyo mikataba na barua ambayo pia inaongeza gharama kwa mfanyabiashara kwa sababu mfumo huo haukuwa rafiki kabisa ndiyo maana utakuta hapa katikati watu walikuwa wananunua mashine za EFD kazi zao ilikuwa ni kuuza risiti na siyo bidhaa tena ila kwa sababu waliona kuna mwanya na fursa ipo kimsingi ni sheria ambayo ilitutesa sana," alisema Msigala.

Baadhi ya wafanyabiashara wa mbao mjini Makambako akiwamo Imani Kifanga alisema licha ya TRA kuondoa utaratibu huo ambao uliwasababishia kero nyingi kutokana na wakulima kutokuwa na mashine za EFD bado inatakiwa kufanyia kazi matatizo mengine hasa za kutozwa ushuru.




Balozi wa Kampeni ya Kidijitali ya Tap Tap Utoboe ya Benki ya Exim Tanzania, Idris Sultan (katikati), akitangaza washindi 10 wa droo ya pili ya mwezi, jijini Dar es Salaam hivi karibuni, yenye lengo la kuwahamasisha wateja wake kufanya miamala ya malipo kwa kutumia simu za mkononi na mtandao. Kushoto ni Ofisa wa Idara ya Huduma Mbadala za kibenki na Kidijitali wa benki hiyo, Thuweiba Bakary na Mkaguzi kutoka Bodi ya Michezo ya Kubahatisha Tanzania, Lucy Katamba. **PICHA: MIRAJI MSALA**

# RC Mtaka asisitiza ubora miradi ya maendeleo

**Na Elizabeth John,** NJOMBE

WATAALAMU mkoani Njombe wametakiwa kutodhalilisha taaluma zao kwa kuharibu miradi ambayo imeletwa na serikali, badala yake wafanye kazi kwa kuzingatia maadili.

Agizo hilo lilitolewa juzi na Mkuu wa Mkoa wa Njombe, Anthony Mtaka, wakati wa ziara ya kutembelea majengo mapya ya Shule ya Msingi Umago iliyopo Kata ya Uwemba yanayojengwa na Mfuko wa Maendeleo ya Jamii (TASAF).

Mtaka alisema Rais Samia Suluhu Hassan ametimiza wajibu wa kuleta fedha za miradi, hivyo kila mmoja anapaswa kutimiza wajibu kwa kuleta matokeo bora na yenye tija.

"Malengo ya hizo pesa ni huduma za wananchi ili ziweze kupatikana kwa wakati, viongozi waliopo kwenye maeneo ya mamlaka ya serikali za mitaa wajibu wao ni kusimamia fedha zinazokuja," alisema Mtaka.

Mtaka alisema mkoa huo hivi sasa umeondokana na kampeni ya kufuta alama sifuri kwenye mitihani ya kidato cha sita.

"Tunachofuta sasa ni utoro kwenye shule, kwa sababu haiwezekani serikali ijenge madarasa, iweke madawati, ilete vitabu, iajiri walimu bado kuna mzazi karne ya 21 hapeleki mtoto shule mpaka apelekwe polisi, tutoke kwenye maisha ya aina hiyo," alisema Mtaka.

Mhandisi wa ujenzi kutoka Halmashauri ya Mji wa Njombe, Bernadetha Mihambo, alisema ujenzi wa majengo ya madarasa mapya, vyoo, nyumba za walimu, bwalo la chakula pamoja na uzio umejengwa kwa gharama ya zaidi ya Sh. bilioni moja.

Mkuu wa Wilaya ya Njombe, Kissa Kasongwa, alisema shule hiyo imejengwa kutokana na tatizo lililokuwapo katika kata hiyo ya kuwa na shule moja ya msingi hali iliyokuwa inasababisha wanafunzi kutembea umbali mrefu.

Aidha, alitumia fursa hiyo kuwataka wazazi kuwachunga watoto kwa kuhakikisha wanavaa mavazi ambayo yanaweza kuwakinga na baridi.

Baadhi ya wananchi wa Kata ya Uwemba walisema wanafunzi walikuwa wanakabiliwa na tatizo la kutembea umbali mrefu kutoka kijiji kimoja hadi kingine kufuata elimu.

Alisema: "Umbali huo ulikuwa unasababisha watoto kuwa watoro hivyo tukakubaliana kuanzisha shule mpya na TASAF wakatusaidia na baada ya hapo tumekomesha tatizo la utoro."

# Wapewa mbinu kukabili majanga ya moto

**Na Elizabeth John,**
NJOMBE

WANANCHI wa Halmashauri ya Mji wa Makambako wilayani Njombe wametakiwa kuchukua tahadhari ya majanga ya moto kwa kuhakikisha wanazima swichi za umeme, majiko ya mkaa na gesi pindi wanapoondoka nyumbani kwenda kwenye shughuli zao za kiuchumi.

Wito huo ulitolewa juzi na Mkuu wa Jeshi la Zimamoto na Uokoaji Makambako, Shaban Kissango wakati akizungumza na waandishi wa habari mjini hapa.

Kissango alisema kumekuwapo na matukio ya moto ambayo yanasababishwa na kuachwa kwa jiko la mkaa likiwa na moto ndani, huku akiwataka wananchi kuzingatia taratibu za ujenzi wa nyumba ili kujiepusha na majanga ya moto pindi yanapojitokeza.

"Nishauri wananchi pale wanapokuwa wanatoka nyumbani wahakikishe wanazima vitu vyote vyenye viashiria na pia upangaji wa vitu ndani vikirundikwa kukitokea majanga inakuwa shida katika uokoaji," alisema Kissango.

Ofisa Habari wa Jeshi la Zimamoto na Uokoaji, Nyerere Mtongori, aliwataka wananchi kutoa taarifa sahihi na kwa wakati pindi wanapokutana na majanga mbalimbali ili wapate msaada wa haraka.

Alisema: "Inatakiwa kama unajua kuna eneo fulani gari letu linatakiwa kupita basi wajitahidi kukaa barabarani ili kutupa uelekeo wa tatizo lilipotokea"



# Dk. Mwinyi ataja kinachoiangusha sekta ya anga

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

RAIS wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi amesema licha ya serikali kupiga hatua katika kuimarisha sekta ya anga, lakini sekta hiyo bado inakabiliwa na changamoto ya usafirishaji wa bidhaa nje ya nchi.

Alisema hayo juzi wakati wa hafla ya uzinduzi wa ndege mpya aina ya Boeing 787-8 Dreamliner iliyowasili juzi visiwani Zanzibar katika Uwanja wa Ndege wa Abeid Amani Karume.

Hivyo aliitaka Mamlaka ya Usafiri wa Anga kukamilisha kazi waliyopewa ya kufanya utafiti wa kubaini changamoto za usafirishaji wa mizigo hasa kwa mazao ya kilimo na mifugo yanayozalishwa nchini kwenda kwenye masoko ya kimataifa.

Alisema serikali itaendelea kufanya uwekezaji mkubwa katika sekta ya usafiri wa anga ikiwamo kuiwezesha ATCL, ujenzi wa viwanja vya ndege na ununuzi wa mitambo ya kuongoza ndege na hali ya hewa ili kuhakikisha matumizi salama na yenye tija.

"Kwa hakika uwekezaji unaofanywa ndani ya ATCL kuna mchango mkubwa katika kufungua nchi, ambapo kutawezesha kuunganisha mikoa yote pamoja na kuiunganisha Tanzania na nchi za kikanda na kimataifa" alisema.

Kadhalika, alitaka ATCL kuangalia uwezekano wa kufanya safari za kimataifa kwa wingi zikipitia Zanzibar ili kukuza uchumi na kuvutia watalii.

Pia, aliitaka Wizara ya Uchukuzi kuisimamia ipasavyo bodi na menejimenti ya ATCL ili kuhakikisha ndege zilizonunuliwa zinatumika kibiashara, kuzifanyia matengenezo kwa wakati na kuwa na viwango bora vya kiusalama.

Alisema serikali itaendelea kusimamia sera na sheria za usafiri wa anga ili mashirika mengi ya ndege yafanye safari nchini.

Katibu Mkuu Wizara ya Uchukuzi, Profesa Godius Kahyarara, alisema gharama za ununuzi wa ndege hiyo ni Sh. bilioni 300, na fedha zote zimelipwa na serikali na siyo mkopo.

Aidha, alisema ndege hiyo ilianza safari Agost 19 mwaka huu majira ya saa tisa usiku kwa saa za Afrika Mashariki ikitokea Marekani na inauwezo wa kutembea saa 14 hadi 20 bila ya kusimama.

Alisema ujio wa ndege hiyo utapanua biashara na kuingiza fedha za kigeni, kwamba kwa muda wa miaka mitatu ATCL limeingiza dola za Marekani milioni 182 kutokana na safari zake za ndege.

Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi Zanzibar, Dk. Khalid Salum, alisema alisema miongoni mwa jitihada za Serikali ya Zanzibar ni kuimarisha huduma za anga kwa kufanya utekelezaji wa miundombinu katika Uwanja wa Ndege wa Abeid Amani Karume. Hivyo, baada ya kukamilika utakuwa na uwezo wa kupokea abiria milioni 300 kwa mwaka.

Alisema ndege hiyo inauwezo wa kubeba abiria 262, inaviti 22 vya daraja la biashara na viti 240 daraja la kawaida, pia ina uwezo wa kubeba mizigo kati ya tani 15 hadi 20 kulingana na ujazo wa abiria na mizigo yao.

## Chuo Kikuu Iringa chapewa heshima Tamasha Kizimkazi

**Na Mwandishi Wetu**

CHUO Kikuu cha Iringa kimepewa heshima ya kuwa msimamizi mkuu wa mafunzo na kutunukia vyeti wahitimu 607 katika wiki la Kizimkazi visiwani Zanzibar.

Vyeti hivyo vilikabidhiwa juzi katika hafla ya kufunga mafunzo ya Tamasha la Kizimkazi iliyofanyika Wilaya ya Kusini Mkoa wa Kusini Unguja.

Mwenyekiti wa Bodi wa chuo hicho, Lilian Badi alisema pamoja na wadau wengine wa maendeleo, Chuo Kikuu cha Iringa kimefundisha na kutunukia vijana hao ambao wamehitimu katika nyanja mbalimbali ikiwamo uvuvi, ufugaji, utalii, ukulima, usanii na ujasiriamali.

Alisema vijana hao wataendelea kulelewa na maendeleo yao kupimwa, ili kujua jinsi gani Tamasha la Kizimkazi linaleta tija kwa wanachi.

Lilian alisema pia vijana hao watawezeshwa zaidi ikiwa watahitaji mitaji na taaluma zaidi katika maeneo yao.

Alisema Chuo Kikuu cha Iringa kimekuwa kinara katika kutoa elimu ya ujasiriamali na mafunzo kwa vitendo Nyanda za Juu Kusini.

"Hii ni kupitia kituo chake cha ujasiriamali ambacho kinaongoza programu iitwayo "Team Academy". Katika programu hii wanafunzi na vijana kutoka maeneo ya jirani hufundishwa mbinu za biashara kupitia mawazo ya biashara (mawazo bunifu) au biashara changa chini ya makocha bobezi," alisema.

Alisema programu hiyo imevuta vijana kutoka maeneo mbalimbali ambao wamefanikiwa kukuza mawazo yao bunifu kuwa biashara halisi ambazo zinafanya vizuri katika jamii.

Kadhalika, alimshukuru Rais Samia Suluhu Hassan kwa kuwa kiongozi mahili anayeshiriki katika kujenga uwezo wa wananchi.



Rais wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi, akiwa na mkewe Mama Mariam Mwinyi, kwenye chumba cha marubani wa ndege mpya ya ATCL Boeing 787-8 Dreamliner wakipata maelezo kutoka kwa Rubani Raymond Musingi, baada ya kuipokea ndege hiyo, katika Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Abeid Amani Karume Zanzibar juzi usiku, akimwakilisha Rais Dk. Samia Suluhu Hassan. **PICHA: IKULU**

# Serikali: Tutashirikiana na wadau kusaidia wakulima

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

MKURUGENZI wa Wakala wa Serikali wa Huduma za Matrekta na Zana za kilimo, Saleh Mohamed Juma, amesema serikali itaendelea kushirikiana na washirika wa maendeleo katika kuwasaidia wakulima ili kuongeza uzalishaji wa chakula nchini na kujipatia kipato.

Alisema hayo Kinyasini, Wilaya ya Kaskazini 'A' Unguja wakati akifungua kikao kinachohusiana na mradi wa uvumilivu wa mfumo wa chakula kwa vijana kwa ajili ya kuwapatia taaluma na uelewa juu ya matumizi bora ya zana za kilimo.

Saleh alisema mwelekeo wa serikali umo katika kuwashajiisha vijana ili waondokane na vitendo viovu na badala yake wajikite katika kufanya kazi za kilimo.

Aidha, alisema taasisi yao itahusika katika kuwashajiisha vijana kuwajengea uwezo wa kitaaluma na kuwasaidia kupata mikopo kwa ajili ya kununulia zana za kilimo baada ya kupata taaluma itakayowasaidia katika kuwahudumia wakulima.

Mwenyekiti wa Bonde la Umwagiliaji Kibokwa, Ukasha Hamdu Juma, aliishukuru serikali kwa kuwawezesha vijana katika kuwapatia elimu ya uchumi na kuondokana na maisha tegemezi ya kukaa katika vijiwe visivyoleta tija.

Sheha wa Kikobweni, Mcha Ali Mcha, alisema mradi huo utawasaidia katika kuwanyanyua vijana na kuwasaidia wazee kwa kushiriki katika shughuli za kilimo, hivyo aliwaomba vijana kuunga mkono mradi ili kujiendeleza kimaisha na kupata riziki zao za halali.

Mkuu wa Bonde la Umwagiliaji Kibokwa, Maryam Mohamed Mwalim, alitoa wito kwa wakulima wawe na muamko wa kwenda kuwashajiisha vijana ili kuingia katika mchakato na kuitumia vizuri fursa iliyopo ambayo itawasaidia kupata ajira endelevu sambamba na kupata ujuzi.

Alisema mradi huo unafadhiliwa na Benki ya Dunia (WB), utawapatia taaluma vijana wa Unguja na Pemba.

# Nchemba aihakikishia Jumuiya ya Madola maboresho mifumo kodi

**Na Benny Mwaipaja**

WAZIRI wa Fedha, Dk. Mwigulu Nchemba, ameihakikishia Jumuiya ya Kimataifa na Watanzania kwa ujumla kwamba serikali inaendelea kuweka na kuboresha mazingira ya uwekezaji ikiwamo kuboresha mifumo yake ya kodi.

Dk. Nchemba aliyasema hayo jana jijini Dar es Salaam, wakati akiagana na Balozi wa Uswisi aliyemaliza muda wake wa ubalozi hapa nchini, Didier Chassot.

Alisema Rais Samia Suluhu Hassan, ameunda timu ya wataalamu ya kupitia na kuja na mapendekezo yatakayosaidia kuboresha mifumo yake ya kodi ili kuvutia zaidi biashara na uwekezaji nchini.

Alifafanua kuwa, pamoja na kuundwa kwa timu hiyo, serikali imechukua hatua kadhaa za maboresho ya kielektroniki ya ukusanyaji kodi yanayosaidia kukusanya mapato yake kwa ufanisi na kuondoa usumbufu kwa walipa kodi.

Dk. Nchemba alisema kuwa, lengo la kuweka mazingira mazuri ya uwekezaji pamoja na kuimarisha mifumo ya kodi ni kuhakikisha kuwa idadi ya walipakodi inaongezeka, hatua itakayosaidia pia kuiwezesha serikali kupunguza viwango vya kodi ya ongezeko la thamani siku za usoni kwa sababu walipakodi watakuwa wengi.

Balozi wa Uswisi aliyemaliza muda wake nchini, Chassot, alipongeza serikali kwa uamuzi huo wa kupitia mifumo ya kodi na anaamini mabalozi wanaoziwakilisha nchi zao hapa nchini, watapata pia nafasi ya kuzungumza na kujadiliana na serikali kuhusu masuala hayo kama walivyoomba.

Balozi Chassot alimwaga Waziri Dk. Nchemba na kuipongeza Serikali ya Awamu ya Sita kwa hatua kubwa iliyopiga kimaendeleo katika kipindi kifupi.

Aidha, aliahidi kuwa Uswisi inaandaa mpango mpya wa ushirikiano wa kimaendeleo na Tanzania utakaojielekeza katika kufanikisha agenda mbalimbali za maendeleo ya nchi kupitia programu zake mbalimbali ikiwamo kusaidia Mfuko wa Maendeleo ya Jamii (TASAF), usimamizi wa fedha za umma, biashara na uwekezaji kupitia asasi za kiraia na sekta binafsi.

Chassot ambaye amekuwa nchini kwa kipindi cha miaka minne ameahidi kuendelea kuwa balozi mzuri wa Tanzania atakaporejea nchini kwake kuendelea na majukumu yake mengine.



Wajumbe wa Kamati ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa wa Baraza la Wawakilishi Zanzibar, wakiwasili kwenye ofisi za Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira (NEMC), kujifunza shughuli za baraza hilo, jana. **PICHA: JOSEPH MWENDAPOLE**

## RC alia na wanaokwepa kuandika wosia

**Na Mwandishi wetu, MTWARA**

MKUU wa Mkoa wa Mtwara, Kanali Patrick Sawala ameagiza Makatibu Tawala wa Wilaya na Maofisa Ustawi wa Jamii katika halmashauri zote za mikoa ya Lindi, Mtwara na Ruvuma kuhamasisha wananchi kuandika wosia ili kupunguza malalamiko na migogoro inayoweza kuepukika kwa warithi pindi wazazi au wategemewa wanapofariki dunia.

Akizungumza wakati wa kufungua mafunzo kuhusu huduma zinazotolewa na Wakala wa Usajili, Ufilisi na Udhamini (RITA) kwa wadau wa usajili katika mikoa hiyo, Kanali Sawala alisema lengo la mafunzo hayo ni kuwajengea uwezo zaidi watendaji hao katika huduma wanazotoa kwa wananchi, ikiwamo mirathi, ndoa na talaka.

"Moja ya sababu kubwa ya migogoro inayotokea katika familia ni baadhi ya wazazi kushindwa kuandika wosia kutokana na imani potofu ya kujitabiria vifo," alisema Kanali Sawala na kuongeza kuwa kuandika wosia si uchuro, kuna watu wengi walioandika wosia muda mrefu uliopita na wanaishi.

Alihimiza watumishi kutoa elimu ya kutosha kuhusu umuhimu wa kuandika wosia na kuwashauri na kuwasaidia namna ya kuandaa wosia huo ili kuepuka matatizo yanayoweza kuepukika katika jamii.

Kanali Sawala pia alihimiza wananchi kufanya kazi badala ya kutegemea mali za urithi ili wafaidike, hata kama wao siyo warithi halali kwa kuwa kutasaidia kupunguza migogoro mingi isiyo ya lazima.

Mbali na kupongeza RITA kwa hatua mbalimbali inazochukua, ikiwamo kuwajengea uwezo watoahuduma, mkuu wa mkoa huyo alisema kuanzishwa mfumo wa huduma kwa njia ya mtandao (eRITA) unaowawezesha wananchi kutuma maombi ya kwa njia ya kidijitali bila kwenda ofisi za RITA kumepanua wigo wa upatikanaji huduma na kufikia wananchi wengi zaidi.

"Ninatoa rai kwa RITA kuweka nguvu zaidi katika kuelimisha wananchi umuhimu wa kutumia mfumo wa e-RITA kwani ni rahisi na unampunguzia mtu gharama ya kusafiri," alisisitiza Kanali Sawala.

Kabidhi Wasii Mkuu na Ofisa Mtendaji Mkuu wa RITA, Frank Kanyusi, alisema taasisi yake imekuwa na utaratibu wa kuandaa mafunzo na vikao kwa wadau wa makundi mbalimbali ili kuwapa elimu na kujadiliana nao kuhusu mikakati na kuongeza ufanisi katika kutoa huduma kwa wananchi.

"Mafunzo yaliyotolewa yaliwajengea uwezo watoahuduma wetu hasa katika maeneo ya usajili wa vizazi, vifo, ndoa, talaka na udhamini," alisema Kanyusi na kuongeza kuwa mafunzo yalilenga umuhimu wa takwimu ambazo ni kichocheo muhimu katika kupanga masuala ya uchumi kwa kutoa uhalisia wa mahitaji kwa wakati uliopo na kuwezesha kutoa makadirio ya mbeleni.

Kanyusi alisema mafunzo hayo yametolewa kwa viongozi hao kwa sababu Sheria ya Usajili wa Vizazi na Vifo inamtambua Katibu Tawala wa Wilaya kama Msajili wa Wilaya, hivyo wanahusika moja kwa moja na usajili wa vizazi, vifo, ndoa, pamoja na kufuatilia na kukusanya taarifa za hukumu za talaka katika maeneo yao. Kwa upande wa Maofisa Ustawi wa Jamii, wao walipewa mafunzo hayo kwa sababu wao wanaratibu na kusimamia mpango wa usajili wa watoto wa umri chini ya miaka mitano.

Mratibu wa Mpango wa Usajili wa Watoto chini ya Miaka Mitano kutoka Ofisi ya Rais - Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Mariam Nkumbwa, alisema kuwa kupitia mafunzo hayo yaliyotolewa na RITA, wanaamini usajili na uingizaji taarifa katika mfumo wa usajili utaboreshwa na kufikia malengo waliyojiwekea.

Katibu Tawala wa Wilaya ya Newala, Thomas Safari, alisema mafunzo hayo yamekuja wakati sahihi kwa kuwa yatasaidia kuwafanya maofisa kufanya kazi zao kwa ufanisi kwa kufuata sheria, kanuni na miongozo inayotolewa na RITA.

## H'shauri Kibaha yataka kuendeleza mali za lililokuwa Shirika la Elimu

**Na Julieth Mkireri, KIBAHA**

BARAZA la Halmashauri ya Mji wa Kibaha limeomba serikali kukabidhi mali za Shirika la Elimu Kibaha ambalo limevunjwa hivi karibuni ili waweze kuendeleza sehemu ambazo zimegeuka mapori na kutumika kwa mambo ya uhalifu.

Mwishoni mwa mwaka 2023 serikali iliunganisha mashirika na taasisi 16 na kuvunja mashirika manne likiwamo la Elimu Kibaha lililokuwa linasimamia Shule ya Sekondari ya Wavulana Kibaha, Tumbi, Shule ya Sekondari ya Wasichana Kibaha, Chuo cha Ufundi na Shule ya Msingi Tumbi.

Mwenyekiti wa Halmashauri ya Mji wa Kibaha, Mussa Ndomba, alitoa ombi hilo jana katika kikao cha Baraza la Madiwani kilichofanyika mjini Kibaha.

Alisema baadhi ya maeneo ya shirika hilo yamegeuka mapori yanayotishia usalama wa wananchi.

Pia Ndomba alisema wapo watu wameanza kuvamia baadhi ya maeneo ya shirika hilo na kuanza kujenga makazi na kuhatarisha wavamizi kuongezeka na kuleta migongano.

"Tunamwomba Rais kupitia Waziri wa Tamisemi watukabidhi mali za shirika ili tuendeleze tuweke hali ya usalama, lakini kuongeza vyanzo vya mapato," alisema.

Kadhalika, Baraza hilo limeelezea kero ya maji ya muda mrefu katika Kata ya Viziwaziwa na Pangani huku wakiomba miradi ya maji kutekelezwa kwa wakati kuwaondolea adha wananchi.

Diwani wa Mbwawa, Judith Muluge, aliomba uhakiki wa mipaka kwenye kata za pembezoni mwa halmashauri ili kuondoa sintofahamu kwa wananchi wa maeneo ya mpakani.

Mkurugenzi wa Halmashauri ya Mji wa Kibaha, Rogers Shemwelekwa, alisema mapato ya halmashauri yameendelea kuongezeka kutokana na ushirikiano baina ya watumishi.

Shemwelekwa alisema kwa mwaka wa fedha uliopita mapato yalikusanywa kwa asilimia 108 na wataendelea kuimarisha makusanyo ili yaweze kutumika kutekeleza miradi ya wakazi wa Kibaha.


**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA TANZANIA**

**Katika Mahakama ya Mwanzo ya Wilaya ya DODOMA**

**Kituo cha MAKOLE Mkoa DODOMA**

**Shauri la Madai Na. 94/2024**

**JINA LA MDAI ........... FRIDA JOHN MAGANGA**

**JINA LA MDAIWA .................... DANIEL CHRISTOPHER SAGAYA**

**KUITWA SHAURINI MDAIWA**
**(Kanuniya 18 yakanunizataratibuMadaikatikaMahakamazaMwanzo)**

**KWA**
**DANIEL CHRISTOPHER SAGAYA**
**IHUMWA - DODOMA**

Kwa kuwa mdai ameleta madai yake kwamba
MADAI YA TSH. 15,000,000/=(Shilingi milioni kumi na tano tu.
Kwa hiyo unatakiwakuhudhuria binafsi katika Mahakama hii tarehe 28 mwezi 08 mwaka2024saa 2:30 asubuhi,
kwa mujibu wa madai hayo na kwa kuwa siku hiyo ni siku ya kusikilizwa shauri hili ni lazima keleta shahidi/Mashahidi wako na vielelezo vyote vinavyohusu shauri hili kwa ajil iya kujitetea.
**ANGALIZO:** Kama hautohudhuria siku iliyotajwa hapo juu na ikithibitika kuwa ulipokea hati ya kuitwa shaurini, Mahakama inaweza kusikiliza shauri bila wewe kuwepo.
Hati hii imetolewa kwa Amri na Muhuri wa Mahakama hii leo tarehe **16 Mwezi 08 Mwaka 2024.**

HAKIMU

HAKIMU
MAHAKAMA YA MWANZO
MAKOLE - DODOMA



**FOMU MADAI – 3**

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA TANZANIA**

**KATIKA MAHAKAMA YA MWANZO KYELA MJINI; WILAYA YA KYELA**

**MKOA WA MBEYA KATIKA SHAURI LA TALAKA NO: 16 YA 2024**

**JINA LA MDAI........................................ FASNES MSIGALA**

**JINA LA MDAIWA..................................... MAWAZO MINGA**

**KUITWA SHAURINI MDAIWA**
**(Kanuni ya 18 ya kanuni za taratibu Madai katika Mahakama za Mwanzo)**

**Kwa : MAWAZO MINGA**

**Kwa kuwa mdai ameleta madai yake ya TALAKA**

Kwa hiyo unatakiwa kuhudhuria binafsi katika mahakama hii Tarehe 28 Mwezi 08 Mwaka 2024. Saa 2:00 Asubuhi. Kwa mujibu wa madai hayo na kwa kuwa siku hiyo ni siku ya kusikilizwa shauri hili ni lazima kuleta shahidi/mashahidi wako na vielelezo vyote vinavyohusu shauri hili kwaajili ya kujitetea.
**ANGALIZO**: kama hautohudhuria siku iliyotajwa hapo juu na ikithibitika kuwa ulipokea hati ya kuitwa shaurini, Mahakama inaweza kusikiliza shauri bila yaw ewe kuwepo.
Hati hii imetolewa kwa Amri na Muhuri wa Mahakama hii leo tarehe 12 mwezi 08 mwaka 2024

MAHAKAMA YA MWANZO
WILAYA YA KYELA
KYELA - MJINI

12/08/2024
HAKIMU
HAKIMU MFAWIDHI
MAHAKAMA YA MWANZO
KYELA MJINI

# WHO: Visa Mpox vinaongezeka Afrika

**GENEVA, Uswisi**

SHIRIKA la Afya Duniani (WHO) limesema idadi ya visa vya Mpox vinaendelea kuongezeka Afrika, huku ikieleza kuwa inajua jinsi ya kudhibiti ugonjwa huo ambao umesababisha maambukizi 99,176 na vifo 208 dunia nzima toka 2022, licha ya kusisitiza kwamba zinahitajika juhudi zaidi za kuudhibiti.

Mkurugenzi wa Kanda ya Ulaya ya WHO, Dk. Hans Kluge, alisema jana kuwa miaka miwili iliyopita mpox ilidhibitiwa Ulaya, kutokana na ushirikiano wa moja kwa moja na jumuiya zilizoathirika zaidi za wanaume wanaofanya mapenzi ya jinsia moja baada ya kufanya uchunguzi kutoa ushauri mzuri wa afya ya umma.

Alisema WHO iliweza kudhibiti mlipuko huo kupitia mabadiliko ya tabia na hatua zisizo za kibaguzi za afya ya umma, pamoja na chanjo ya mpox.

Katika hatua nyingine WHO ilisema mpox sio janga jingine jipya kama ilivyokuwa COVID-19, kwa sababu maofisa wanafahamu vizuri kuhusu virusi hivyo na njia ya kujikinga na ugonjwa huo na hatua za kuzuia usienee zinaendelea.

Kwa mujibu wa Kluge, takribani visa 100 vya kirusi kipya vinarekodiwa kwa mwezi barani Ulaya, huku wataalamu wa afya wakisema aina mpya ya kirusi Clade 1b kinaonekana kuambukiza zaidi kuliko aina ya virusi iliyopita, na pia ina uwezekano mkubwa wa kusababisha maambukizo makali.

Msemaji wa WHO, Tarik Jasarevic, alisema shirika hilo halipendekezi matumizi ya barakoa, wala chanjo ya watu wengi. Na kwamba wanapendekeza matumizi ya chanjo katika mazingira ya mlipuko kwa makundi ambayo yako katika hatari zaidi.

Aidha, Agosti 14, mwaka huu, WHO ilitangaza hali ya dharura ya afya ya umma kimataifa, kutokana na kuongezeka kwa visa vya aina mpya ya kirusi Clade 1b katika Jamhuri ya Kidemokarsi ya Kongo (DRC) na kuenea kwake kwenye nchi jirani.

Wakati huo huo, Mkurugenzi Mkuu wa Kituo cha Kuzuia na Kudhibiti Magonjwa barani Afrika, (CDC) Jean Kaseya, alisema mazungumzo tayari yameanza na kampuni ya madawa ya Denmark ya Bavarian Nordic kuhusu upelekaji wa teknolojia yake mpya ya chanjo za mpox, ili iweze kutengenezwa barani Afrika katika siku zijazo.

Naye Mkurugenzi Mkuu wa Bavarian Nordic, Paul Chaplin alisema kampuni hiyo inaweza kuongeza uzalishaji wa chanjo yake ya mpox hata kabla ya kupokea oda, lakini hilo litategemeana matokeo ya mkutano wake na WHO utakaofanyika wiki hii.

***DW***



Wafanyakazi wengi wa nyumbani wakiwamo wanaotoka nchini Kenya waliokuwa wakifanya kazi Ethiopia wamepoteza kazi zao wakati wa msukosuko wa kifedha wa Lebanon, huku wakiomba msaada wa kurudishwa nyumbani. **PICHA: MTANDAO**

# Mbaroni baada ya mafuvu 17 kupatikana ndani kwake

**KAMPALA, Uganda**

MAOFISA wa Jeshi la Polisi nchini Uganda wamemkamata mwanamume mmoja aliyetambulika kwa jina la Lujja Tabula baada ya kupatikana kwa mafuvu 17 ya vichwa vya binadamu katika kaburi moja lililokuwa kwenye chumba cha chini ndani ya makazi yake.

Ilielezwa kuwa Julai 28, mwaka huu wanakijiji walioshtuka walishuhudia mabaki hayo, ambayo polisi wakati huo walisema ni pamoja na mafuvu matatu ya watoto, katika chumba kilichoko chini ya ardhi katika mji wa Mpigi, uliopo magharibi mwa Kampala.

Msemaji wa Polisi Kituuma Rusoke, alisema kikosi cha polisi cha upelelezi wa uhalifu kilipata taarifa na kumkamata Tabula Agosti 19, mwaka huu na kwamba yuko kizuizini.

"Tabula alikuwa akitafutwa kuhusiana na mafuvu ya vichwa vya binadamu viliyokutwa katika makazi yake huko Mpigi hivi karibuni, na atafikishwa mahakamani upelelezi utakapokamilika," alisema. Bado haijulikani jinsi mafuvu ya kichwa yaliishia sehemu hiyo, iliyoko kwenye juu ya mlima, na iliyozikwa ndani ya masanduku manne ya chuma ndani ya chumba kilicho chini ya ardhi kwa undani wa mita mbili.

Vyombo vya habari vya eneo hilo viliripoti wakazi wakisema kwamba watu walikuwa wamekusanyika hapo awali kuabudu.

Tabula pia alikuwa akitafutwa na polisi kuhusiana na kesi tofauti inayohusu mauaji ya kiongozi maarufu wa kimila wa Baganda, mjasiriamali Daniel Bbosa, na alikuwa akitoroka kabla ya kugunduliwa kwa mafuvu hayo.

Mauaji hayo mjini Kampala yaliripotiwa kutekelezwa na watu waliokuwa wamejihami kwa bunduki wakati Bbosa akirejea nyumbani kutoka kazini Februari mwaka huu.

***TRT***

# Obama: Marekani iko tayari kwa urais wa Kamala

**NEW YORK, Marekani**

RAIS wa zamani wa Marekani, Barack Obama, amewaambia wanachama wenzake wa Chama cha Democratic mjini Chicago kuwa kijiti kimekabidhiwa rasmi kwa Kamala Harris, na taifa hilo liko tayari kwa uongozi wake kwa sababu anatosha kulionGoza taifa hilo.

Akihutubia wakati wa kumpigia debe Kamala katika mkutano mkuu wa Chama cha Democratic, jana Obama alisema Harris ambaye kwa sasa ni Makamu wa Rais wa Marekani, ndiye atawapigania Wamarekani.

Alisema Kamala yuko tayari kwa ajili ya kazi ya urais, na amekuwa akiyatumia maisha yake kuwapigania watu wasio na sauti huku akitoa wito kwa Wamarekani kujitokeza kwa wingi siku ya uchaguzi wa Novemba mwaka huu ili kumshinda Donald Trump.

Pia Obama aliwaambia Wanademokrasia waepuke 'upumbavu' wa kusubiri kuombwa kuchukua hatua na alitoa wito wa kibinafsi kwa kila mtu kufanya kitu kati ya sasa na siku ya Uchaguzi.

"Ndiyo, Kamala na Tim wanafanya vyema sasa, tunaipenda, wanapakia viwanja kote nchini, watu wanatiwa nguvu, tunajisikia vizuri. Lakini kumbuka, bado kuna watu wengi ambao wanatamani matokeo tofauti," alisema Oboma.

Aliweka wazi vigingi, na changamoto, zinazomkabili Harris kama mwanamke mweusi anayetafuta ofisi ya juu zaidi kuliko msemaji mwingine yeyote wa mkutano hadi sasa. akigusia miaka ambayo Trump alitumia kueneza njama ya uwongo, ya ubaguzi wa rangi.

„Nani atamwambia kuwa kazi anayotafuta kwa sasa inaweza kuwa moja ya kazi hizo za Weusi," alisema.

Giles ambaye ni mmoja wa wanachama wa chama hicho alisema „Nina ujumbe wa dharura kwa Wamarekani wengi ambao, kama mimi, wako katikati ya kisiasa: Chama cha Republican cha John McCain kimeondoka, na hatuna deni kubwa kwa kile ambacho kimeachwa. Kwa hivyo wacha tufungue ukurasa. Tutangulize nchi mbele".

Hotuba ya Giles ilihitimisha kwa kukaribisha msururu wa watu ambao walikuwa wamekihama chama, wakitafuta uungwaji mkono kwa Harris.

***CNN***

## Don Bosco yapewa vifaa vya michezo

**Na Maulid Mmbaga**

WADAU wa afya nchini wamejitokeza kuunga mkono vijana wa timu za mpira wa kikapu kwa kudhamini na kuwapatia vifaa mbalimbali kwa lengo la kuwasaidia kukuza vipaji na kutimiza ndoto zao kupitia michezo.

Akizungumza jijini Dar es Salaam jana, Ofisa Mtendaji Mkuu wa Jubilee Life Insurance, Helena Mzena, alisema lengo la kutoa udhamini huo kwa timu ya Don Bosco ni kutaka kuona inafanya vyema katika mashindano mbalimbali.

"Tumeamua kudhamini timu hii kwa sababu ni kati ya timu zinazosaidia vijana wa rika tofauti kutimiza malengo na ndoto zao kupitia njia ya michezo, na kutakuwa na mechi tano zitakazoanza hivi karibuni ambazo tutashiriki kuwatia moyo na kuwahamasisha vijana waendelee kufanya vizuri katika mashindano mbalimbali wanayoshiriki," alisema Helena.

Aliongeza kuwa, udhamini huo utakuwa endelevu na hawataangalia gharama badala yake wataangalia matokeo chanya watakayopata vijana hao katika msingi wa kukuza vipaji vyao.

Mlezi wa timu hiyo, Joachim Sivali, aliwashukuru wadau hao kwa kukubali ombi la kuwadhamini na kusema Jubilee Life wamefanya hivyo kwa sababu wanafahamu michezo inadumisha afya.

## Kibago ajitabiria makubwa BAMATA

**Na Shufaa Lyimo**

NAHODHA wa Kombaini ya Timu ya Jeshi la Wananchi Tanzania (Lugalo) kwa upande wa mchezo wa vishale, Kamdas Kibago, amesema wanaendelea vyema na mazoezi kwa ajili ya kufanya vizuri katika mashindano ya Majeshi (BAMATA) yatakayofanyika kuanzia Septemba 6, mwaka huu mkoani, Morogoro.

Akizungumza na gazeti hili jana, Kibago, alisema malengo yao ni kupata ubingwa katika mashindano hayo ambayo yanatarajiwa yatakuwa na upinzani mkubwa.

"Tunaendelea kufanya mazoezi kwa ajili ya kujiandaa na mashindano ya BAMATA, tunataka kuwa mabingwa mwaka huu na tunauhakika tutafikia malengo kutokana na mazoezi tunayofanya," alisema Kibago.

Amewataka Watanzania kujifunza mchezo huo kwa sababu una faida kama ilivyo michezo mingine inayochezwa hapa nchini.

"Ninaomba Watanzania wenzangu wajitokeze kwa wingi kujifunza huu mchezo kwa sababu utawasaidia kupata ajira na kujitangaza kwa watu huku pia itawafungulia fursa mbalimbali, „alisema nahodha huyo.

# KMC FC YAFUNGUKA AWESU, WAZIRI JR WAMEACHA PENGO

**Na Faustine Feliciane**

WAKATI Kocha wa KMC, Abdihamid Moallin, akisema kikosi chake kina kazi kubwa ya kupambana ili kumaliza nafasi za juu katika Ligi Kuu Tanzania Bara msimu huu, ameweka wazi kuondoka kwa nyota wake wawili, Awesu Awesu na Waziri Junior, kumewaachia pengo.

Awesu amejiunga na Simba huku akifunga bao la tatu katika ushindi wa magoli 3-0 wakati wakicheza dhidi ya Tabora United wakati Waziri amesajiliwa na Dodoma Jiji FC.

Akizungumza jijini Dar es Salaam jana, Moallin, alisema ataendelea kuwajenga wachezaji wake kuonyesha kiwango bora ingawa haitakuwa kazi rahisi kutokana na kikosi chake kupunguzwa nguvu.

Moallin alisema wanaendelea kuwajengea uwezo wachezaji waliopo ili wasitetereke na hatimaye kufikia malengo ya timu yao.

"Mpira una changamoto zake katika kujenga kikosi, unaweza ukawa na wachezaji wazuri wakaondoka, kama kocha lazima ufanye kazi yako kuhakikisha timu inakuwa imara na inapambania malengo yake," alisema kocha huyo wa zamani wa Azam FC.

Aliongeza, ligi ni ngumu hivyo anaendelea kukiimarisha kikosi chake na kutodharau mchezo wowote.

"Ligi ni kama marathon, ni lazima kupambana bila kuchoka, tunataka kumaliza katika nafasi nzuri, nawaamini wachezaji wangu," Moallin alisema.

Aliongeza wanatarajia wataonyesha kiwango kizuri katika mechi yao ya Ligi Kuu Tanzania Bara dhidi ya Coastal Union itakayochezwa Agosti 29, mwaka huu licha ya kuwa na changamoto ya mabadiliko ya kikosi chake.

"Lengo letu tufanye vyema kuliko msimu uliopita, ingawa si rahisi, timu zimejiandaa sana msimu huu. Tuliifanya timu iwe katika tano bora msimu uliopita, msimu huu tumefanya maandalizi mazuri, tumefanya usajili wa wachezaji tuliokuwa tunawahitaji, tena wanaocheza kwa staili yetu ya uchezaji, nadhani tutafanikiwa, kama tulimaliza nafasi ya tano, lengo ni kupata nafasi hiyo tena au ya nne," aliongeza kocha huyo.

Yanga ndio mabingwa watetezi wa ligi hiyo inayoshirikisha timu 16 kutoka mikoa mbalimbali ya Tanzania Bara.



Wachezaji wa Azam FC wakifanya mazoezi kwa ajili ya kujiandaa na mechi ya marudiano ya mashindano ya kimataifa ya Ligi ya Mabingwa Afrika dhidi ya wenyeji APR itakayochezwa Jumamosi kwenye Uwanja wa Amahoro jijini Kigali, Rwanda. **PICHA: AZAM FC**

## JWTZ lapongezwa kuenzi sanaa

**Na Faustine Feliciane**

SHAMRASHAMRA za maadhimisho ya miaka 60 ya Jeshi la Wananchi Tanzania (JWTZ) zinaendelea baada ya Naibu Waziri wa Utamaduni, Sanaa na Michezo, Hamis Mwinjuma (Mwana FA), kufungua mashindano ya utamaduni ya Mkuu wa Majeshi ya Ulinzi (CDF).

Mashindano hayo yameanzishwa kwa mara ya kwanza mwaka huu na CDF, Jenerali, John Mkunda yakishirikisha bendi za muziki 10, vikundi vya ngoma na utamaduni tisa vyote kutoka JWTZ.

Akifungua mashindano hayo juzi jijini Dar es Salaam, Naibu Waziri Mwinjuma alisema, anampongeza CDF kwa kuanzisha mashindano hayo ikiwa ni kufanyia kazi maelekezo ya Rais Dk. Samia Suluhu Hassan kuhusu kuendeleza sanaa ya utamaduni na kuulinda.

**"Tunasahau sisi ni nani, tuna sahau utamaduni wetu, nam pongeza sana CDF kwa kulifany ia kazi hili na kurudisha sanaa na utamaduni wetu ni sehemu ya kuulinda usipotee" alisema Mwana FA.**

Mwenyekiti wa Kamati ya mashindano hayo, Meja Jenerali Mbaraka Mkeremy, alisema lengo la CDF ni kurejesha sanaa ya utamaduni ikiwa ni sehemu ya kuelimisha vijana na kuwakumbusha asili ya Watanzania.

Mkeremy alivitaja baadhi ya vikundi vilivyoshiriki ni Nyuki Jazz kutoka Zanzibar, Mlale Jazz, Mwenge Jazz, Air Jazz, JKT Kimbunga, Ruvu Stars, Mbweni Jazz ‚Wazee wa Jodari', Makutopora Jazz , Matajiri wa Zabibu', Mpwapwa Jazz na TMA Jazz.

Katibu Mtendaji wa Baraza la Sanaa Tanzania (BASATA), Dk. Kedmom Mapana, alisema sanaa na utamaduni si burudani bali ni biashara, baraza hilo linawakaribisha wanaotaka kuwekeza katika tasnia hiyo.

## ZISIKUPITE

### GUNDOGAN KURUDI EPL

KLABU ya Manchester City iko mstari wa mbele kumsajili kiungo wa zamani wa Ujerumani, Ilkay Gundogan, kutoka Barcelona, huku mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 33 akitanguliza kurejea Ligi Kuu England. ***(Athletic)***

### SANCHO ATAJWA CHELSEA

CHELSEA inaweza kuchelewa kumsajili mshambuliaji wa Manchester United na Timu ya Taifa ya England, Jadon Sancho, mwenye umri wa miaka 24. ***(Athletic)***

### MAMADASGVILI SOKONI

LIVERPOOL imewasilisha ofa iliyoboreshwa ya pauni milioni 34 kwa mlinda lango wa Valencia na Timu ya Taifa ya Georgia, Giorgi Mamadashvili, mwenye umri wa miaka 23. ***(Relevo)***

### UGARTE ANUKIA UNITED

KLABU ya Paris St-Germain imewapa Manchester United nafasi ya kumsajili kiungo wa kati wa Timu ya Taifa ya Uruguay, Manuel Ugarte, mwenye umri wa miaka 23 kwa mkopo wa msimu mmoja na jukumu la kumnunua. ***(Telegraph)***

### CANCELO AOTA MBAWA

BARCELONA haiko tayari kumsajili tena beki wa pembeni wa Manchester City na Ureno, Joao Cancelo, mwenye umri wa miaka 30, kwa sababu ya madai yake ya mshahara wa pauni milioni 12. ***(Sport)***

### PELLISTRI KUTUA UGIRIKI

KLABU ya Manchester United imekubali mkataba wenye thamani ya takriban pauni milioni tano kwa winga wa Timu ya Taifa ya Uruguay, Facundo Pellistri, mwenye umei wa miaka 22, kujiunga na klabu ya Ugiriki ya Panathinaikos. ***(Telegraph)***

### MEJBRI AKARIBIA BURNLEY

KLABU ya Burnley imeonyesha nia ya kumsajili kiungo wa kati wa Manchester United na Timu ya Taifa ya Tunisia, Hannibal Mejbri, mwenye umri wa miaka 21. ***(Athletic)***

### O'SHEA AGOMBEWA ENGLAND

KLABU za Wolves na Brentford zinamtaka mchezaji wa Burnley, Dara O'Shea, mwenye umri wa miaka 25, lakini lazima walipe pauni milioni 15 ili kumsajili beki huyo wa Jamhuri ya Ireland. ***(Mirror)***

### ARSENAL YAIBANIA FOREST

ARSENAL inataka zaidi ya pauni milioni 30 kumuuza mshambuliaji wa England, Eddie Nketiah, mwenye umri wa miaka 25, baada ya kukataa dau la pauni milioni 25 kutoka kwa Nottingham Forest. ***(Football Insider)***

### BERG AKARIBIA LIVERPOOL

KLABU ya Bayer Leverkusen imewasiliana na Liverpool kuhusu uwezekano wa kumnunua Sepp van den Berg huku Wekundu hao wakitarajiwa kuhitaji pauni milioni 25 kwa mlinzi huyo wa Uholanzi. ***(Florian Plettenberg)***

### MC TOMINAY KIMEELEWEKA

MANCHESTER United iko tayari kumuuza kiungo wa Scotland, Scott McTominay, mwenye umri wa miaka 27 kwa Napoli ili kufuata kanuni za Financial Fair Play (FFP). ***(Corriere dello Sport)***

# DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA




# MBAPPE AIFUNGULIA KESI YA MADAI PSG

Mshambuliaji huyo ataka kulipwa Euro milioni 55 huku vigogo hao...

**PARIS, Ufaransa**

KYLIAN Mbappe amechukua hatua za kisheria dhidi ya waajiri wake wa zamani Paris Saint-Germain huku akitaka kulipwa kitita cha Euro milioni 55, kwa mujibu wa ripoti.

Mbappe aliondoka PSG kwa uhamisho wa bure msimu huu wa joto na kutua Real Madrid, lakini amekuwa kwenye mzozo na klabu hiyo ya zamani kuhusu kile anachoamini ni mishahara ambayo hajalipwa na bonasi za uaminifu tangu alipokuwa Paris.

Mbappe anadai hakulipwa kwa miezi mitatu ya mwisho pale PSG, huku pia akisisitiza bado hajapokea sehemu ya malipo ya bonasi katika mkataba wake.

Kama ilivyofichuliwa kwa mara ya kwanza na Le Monde, Mbappe sasa amewaamuru wawakilishi wake wawasiliane na idara ya sheria ya bodi inayosimamia soka ya Ufaransa (LFP), pamoja na UEFA, kutaka alipwe madai hayo.

Ilifichuliwa mnamo Juni, mwaka huu wawakilishi wa Mbappe walikuwa wameionya PSG watafuata hatua za kisheria.

Klabu hiyo ya Ufaransa ilisisitiza "mazungumzo yalikuwa yanaendelea" lakini, bila azimio lililopatikana hadi sasa, fowadi huyo wa Madrid amechagua kupeleka mambo katika ngazi nyingine.

Mapema mwezi huu, kambi ya Mbappe iliwasiliana na LFP kuhusu mishahara ambayo haijalipwa, ikiangazia sheria ambayo inasema klabu lazima ilipe mishahara yao ya kila mwezi kabla ya siku ya mwisho ya mwezi unaohusika.

Ingawa kukosekana kwa malipo kwa miezi mitatu husika kunaweza kuonekana kama hitimisho la kukata na shoka, PSG wanaendelea kubishana kuwa masharti ya makubaliano ya Mbappe na klabu yalibadilishwa alipoweka wazi ana mpango wa kuondoka klabuni hapo kwa uhamisho wa bure.

Mbappe alifikia makubaliano na Rais wa PSG, Nasser Al Khelaifi, mwanzoni mwa msimu wa 2023/24.

PSG walitaka kumuuza fowadi huyo kabla ya kuhatarisha kumpoteza bila malipo lakini hatimaye Mbappe alikaribishwa kwenye timu baada ya kukubali kukataa baadhi ya fedha anazodaiwa ikiwa angeondoka bure.

PSG wanasisitiza hawana deni la Euro milioni 55 kwa Mbappe kwa sababu ya masharti ya mpango huo mpya, na hivyo LFP na UEFA sasa ndio watakaoamua haki ipo wapi.

# FODEN MCHEZAJI BORA WA MWAKA ENGLAND

**MANCHESTER,** ENGLAND

PHIL Foden amekamilisha tuzo ya mtu binafsi mara mbili kwa kutajwa kuwa Mchezaji Bora wa Mwaka wa Chama cha Soka England kwa mwaka 2024 ikiwa ni miezi mitatu baada ya kushinda tuzo ya Mwanasoka Bora wa Mwaka wa (FWA), kufuatia taji la nne mfululizo la Ligi Kuu England akiwa na Manchester City.

Foden mwenye umri wa miaka 24 amekuwa mchezaji wa nne wa City katika kipindi cha miaka mitano kuchaguliwa kama Mchezaji Bora wa Mwaka, huku Kevin De Bruyne akishinda kati ya mwaka 2020 na 2021, na Erling Haaland (2023).


Mshambuliaji huyo wa England ambaye hapo awali alishinda tuzo ya Mchezaji Bora Chipukizi wa PFA mnamo mwaka 2021 na 2022, alipokea taji la Mchezaji Bora wa Mwaka kwenye chakula cha jioni cha Tuzo za PFA huko Manchester juzi usiku.

Mshambuliaji wa Timu ya wanawake ya Manchester City, Khadija Shaw, alitwaa taji la Mchezaji Bora wa Mwaka wa Wanawake baada ya kuongoza orodha ya wafungaji wa WSL kwa mabao 21 msimu uliopita, mabao nane zaidi ya wapinzani wa karibu Lauren James na Elisabeth Terland.

Kama Foden, Shaw kutoka Jamaika pia alishinda tuzo ya FWA (Chama cha Waandishi wa Soka) kama Mwanasoka Bora wa Mwaka wa Wanawake mwishoni mwa msimu wa 2023-24.

Fowadi wa Chelsea, Cole Palmer alitangazwa mshindi wa tuzo ya Mchezaji Bora Chipukizi wa PFA baada ya kufunga mabao 27 na asisti 15 katika michuano yote katika msimu wake wa kwanza Stamford Bridge kufuatia uhamisho wa pauni milioni 40 kutoka City Agosti mwaka jana.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 22 pia aliingia kwenye kikosi cha England msimu uliopita na kuhitimisha kampeni hiyo kwa kufunga bao katika kichapo cha Fainali ya Euro 2024 dhidi ya Hispania mjini Berlin mnamo Julai.



## Chelsea yajiandaa kumnunua Sancho

**MANCHESTER,** ENGLAND

KLABU ya Manchester United bado iko tayari kumuuza winga Jadon Sancho, huku ripoti ikisema Chelsea inaweza kumnunua mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 24.

Sancho amerejea katika kikosi cha United baada ya mazungumzo mazuri na Kocha, Erik ten Hag kumaliza ugomvi wa wawili hao tangu msimu uliopita, lakini ugonjwa wa sikio ulimfanya kuachwa nje ya timu katika mechi yao ya ufunguzi ya msimu dhidi ya Fulham.

Wakati The Athletic likisisitiza kukosekana kwa Sancho dhidi ya Fulham kulisababisha na majeraha, inabainika United bado iko tayari kumuuza winga huyo kwa bei inayofaa, huku Sancho mwenyewe akiwa na nia ya kutafuta klabu ambayo inaweza kumpa dakika za kutosha.

Paris Saint-Germain walikuwa wametajwa wawaniaji watarajiwa lakini haiaminiki wameendeleza nia yao zaidi ya uchunguzi wa awali, huku dili lao la euro milioni 50 kumsaini Desire Doue kutoka Rennes limemaliza uvumi huo.

Muhimu zaidi, hakuna kutajwa kwa nia yoyote halisi kutoka kwa Chelsea, ambao wanakaribia kukamilisha dili la kumsajili mshambuliaji wa Atletico Madrid, Joao Felix na wana nia ya kumnunua Victor Osimhen wa Napoli kabla ya mwisho wa dirisha la usajili la majira ya kiangazi.

Hapo awali Chelsea walikuwa wakihusishwa na Sancho katika ripoti kutoka Ujerumani mapema mwezi huu, lakini mapendekezo ya mkataba wa mkopo ambao ungewafanya The Blues walipe sehemu kubwa ya mishahara ya Sancho, ambayo ni zaidi ya pauni 250,000 kwa wiki.

United wanasemekana kutafuta ada ya pauni milioni 40 ili kumuuza Sancho, ambayo ingewakilisha hasara ya pauni milioni 33 kwenye ada iliyolipwa ya pauni milioni 73 kumnasa kutoka Borussia Dortmund miaka mitatu iliyopita.

Dortmund wanajulikana kutaka kumsajili tena Sancho lakini waliweka wazi mapema msimu huu wa joto kwamba bei inayotakiwa na United ni kubwa mno wasiweze kuipenda.



## Barcelona yajitosa kumwania Chiesa

**BARCELONA,** HISPANIA

BARCELONA inaripotiwa kuwasiliana na wakala wa winga wa Juventus, Federico Chiesa huku miamba hao wa Katalunya wakijaribu kuongeza safu yao ya ushambuliaji kwa njia rahisi zaidi.

Chiesa ameingia mwaka wa mwisho wa mkataba wake mjini Turin na hajaongezewa tena, na hivyo kulazimisha Juve kumuuza ikiwa wanataka kuepuka kumpoteza mshindi huyo wa Euro 2020 kama mchezaji huru msimu ujao.

Mwandishi Gianluca Di Marzio ameandika Fali Ramadani, mwakilishi wa Chiesa, anawasiliana na viongozi wa Barcelona ili kujadiliana masuala ya kibinafsi.

Baada ya hapo, itakuwa chini ya klabu mbili kuafikiana juu ya ada ya uhamisho ili uhamisho ufanyike.

**Inapendekezwa kuondoka Serie A ndio njia bora zaidi kwa Chiesa, huku chaguzi za yeye kusalia Italia zikieleze wa kuwa „sio thabit i sana“. Chiesa hakuwa chaguo la kwanza la Barcelona kwa winga msimu kwani walikuwa wakimtaka Nico Williams wa Athletic Club, lakini uhaba wa kifedha ulitatiza uwezo wao baada ya kukumbana na matatizo ya kumsajili Dani Olmo.**

Lakini SPORT inaripoti hali ya mkataba wa Chiesa imeibua uwezekano wa kumsajili mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 26 kwa kitita cha euro milioni 14. Anaweza hata kukubali kupunguziwa mshahara wake wa kila mwaka wa euro milioni sita ili kuhamia Barcelona mradi tu mkataba wake uwe wa miaka mitatu.

# SIMBA QUEENS YASONGA MBELE MICHUANO CECAFA

**Na Somoe Ng'itu**

WAWAKILISHI wa Tanzania, Simba Queens wametinga hatua ya nusu fainali ya mashindano ya Klabu Bingwa Afrika Mashariki na Kati kwa Wanawake baada ya kupata ushindi wa mabao 3-0 dhidi ya Kawempe Muslim ya Uganda katika mechi ya Kundi B iliyochezwa kwenye Uwanja wa Abebe Bikila, Ethiopia jana asubuhi.

Kwa ushindi huo, Simba Queens imefikisha pointi sita na kuongoza Kundi B lenye timu za PVB Buyenzi na FAD ya Djibouti.

Mabao ya Simba Queens katika mechi hiyo yote yalifungwa katika kipindi cha pili kupitia kwa Vivian Corazone, Jentrix Shikangwa na Elizabeth Wambui.

Mabingwa hao wa Ligi Kuu ya Wanawake Tanzania (TWPL), Simba Queens watashuka tena dimbani kukamilisha mechi za hatua ya makundi kesho kuvaana na PVB Buyenzi.

Katika mechi yake ya kwanza, Simba Queens ilipata ushindi mnono wa mabao 5-0, nahodha wa zamani wa Twiga Stars, Asha Rashid ‚Mwalala' akifunga hat trick ya kwanza kwenye michuano hiyo inayoandaliwa na kusimamiwa na Baraza la Soka la Afrika Mashariki na Kati (CECAFA).

Wenyeji CBE FC wenye pointi sita tayari wameshasonga mbele katika michuano hiyo kutoka Kundi A baada ya kupata ushindi kwenye mechi zake mbili walizocheza dhidi ya Rayon Sports na Polisi Kenya.

Mechi za hatua ya nusu fainali zitachezwa Jumatatu na fainali ya mashindano hayo itafanyika Agosti 29, mwaka huu.




Wachezaji wa Simba Queens wakishangilia baada ya kufunga bao la kwanza katika mechi ya mashindano ya Klabu Bingwa Afrika Mashariki na Kati (CECAFA), dhidi ya Kawempe Muslim ya Uganda iliyochezwa kwenye Uwanja wa Abebe Bikila jijini Addis Ababa, Ethiopia jana asubuhi. Simba Queens ilishinda mabao 3-0. **PICHA: SIMBA SC**

# Matampi awapa jeuri Coastal

**Na Adam Fungamwango**

WAKATI golikipa tegemeo raia wa Jamhuri ya Kidemokrasi ya Congo, Ley Matampi, akirejea kikosini, Coastal Union imeahidi kupata ushindi mnono katika mechi ya marudiano ya michuano ya kimataifa ya Kombe la Shirikisho Afrika dhidi ya Bravos Do Maquis itakayochezwa Jumapili.

Kocha Mkuu wa timu hiyo, David Ouma, alisema jana kurejea kwa Matampi kumewapa nguvu ya kupambana kupata ushindi ambao utawafanya wasonge mbele katika michuano hiyo.

Ikiwa ugenini nchini Angola, Coastal Union, ilibugizwa mabao 3-0 na hivyo inahitaji ushindi wa kuanzia magoli 4-0 katika mchezo wa marudiano utakaochezwa kwenye Uwanja wa Azam Complex, Dar es Salaam ili isonge mbele.

Kocha huyo alitaja sababu mbalimbali ambazo zilisababisha kupoteza mechi ya kwanza ikiwamo baadhi ya wachezaji wake kuwa majeruhi.

"Hatujakata tamaa, tulifungwa mabao 3-0, tulikuwa ugenini lakini safari hii tutakuwa nyumbani, tunacheza mbele ya mashabiki wetu pamoja na hali ya hewa tuliyoizoea, moja ya vitu ambavyo vilitukwaza ni hali ya hewa, nao pia kwetu wataathirika nalo, ilikuwa baridi kwetu itakuwa ni joto kwao, hivyo tutaitumia faida hiyo kupindua meza," alisema Ouma. Mchezaji Jackson Shiga, naye alisema urejeo wa Matampi langoni, imeamsha ari ya wachezaji kupambana kwani wanajua uwezo wake na jinsi aliyowabeba msimu uliopita.

"Tumerudi nyumbani, mchezo hautakuwa rahisi wala mgumu, kikubwa ni kupata matokeo mazuri na kusonga mbele, kinachotupa nguvu ya kusema hivi ni urejeo wa Matampi, alikuwa na matatizo ya hapa na pale, kila mtu sasa ana imani na kuona mchezo wa Jumapili utakuwa bora sana kwetu," alisema Shiga.

## Yanga, Magoma watinga Korti Kuu

INATOKA UK. 24

hakama kutupilia mbali rufani hiyo.

Jaji Maghimbi baada ya kusikiliza pande zote mbili, wameshapeana nyaraka za shauri hilo, yakiwamo mapingamizi, aliahirisha kesi hadi Agosti 30, mwaka huu kwa ajili ya kusikiliza pingamizi.

Uamuzi wa Mahakama ya Kisutu ulitolewa na Hakimu Mkazi Mfawidhi Franco Kiswaga, aliyesema Bodi ya Yanga iliwasilisha maombi manne ya kuomba kufanya marejeo. Mahakama ilikubali maombi matatu; moja ililitupilia mbali kwa hoja halina mashiko kisheria.

Alisema sababu ya kwanza, bodi inadai Magoma na wenzake walipeleka maombi yao katika mahakama ambayo haina mamlaka ya kuyasikiliza ambayo ni Mahakama ya Kisutu.

Sababu ya pili, mahakama inaona haina mashiko kwa sababu ili mahakama iweze kufanya marejeo, hapaswi kwenda kuangalia ushahidi, suala la kwamba walitakiwa kutoa kadi za uanachama ili kuhalalisha uanachama wao ni suala la ushahidi.

Sababu ya tatu, Magoma na Mwaipopo walitakiwa kufungua shauri la hati ya madai na si maombi kama walivyowasilisha wao, jambo ambalo mahakama imeona ni sababu ya kuikubalia bodi hiyo kufanya marejeo ya shauri hilo.

Alitaja sababu ya nne, baada ya mahakama kupitia kumbukumbu ya shauri namba 187/2022, imebaini Abeid alijitanabaisha yeye ni Mwenyekiti wa Bodi na Fatma Karume alimruhusu amwakilishe mahakamani, jambo ambalo hakuwahi kuruhusiwa kufanya hivyo.

Alisema Abeid hakuwahi kupata idhini kutoka kwa mtu yeyote ya kumsimamia mahakamani na hakujibu chochote kuhusu tuhuma hizo, kwa maana hiyo Bodi ya Wadhamini na Karume hawakuwa na mwakilishi, hivyo walinyimwa haki yao ya kusikilizwa.

Hakimu huyo alisema kwa sababu hizo mahakama inaona maombi ya marejeo yana mashiko, hivyo imekubali Bodi ya Wadhamini ya Klabu ya Yanga kufanya hivyo.

"Mahakama inatupilia mbali mwenendo nzima wa maombi namba 187/2022 yaliyofunguliwa na Magoma na wenzake na kuweka kando amri zote zilizotolewa katika hukumu hiyo pamoja na tuzo iliyolewa Agosti 2, 2023.

"Na kuhusiana na gharama za shauri hili, mahakama inaamuru Magoma, Mwaipopo na Abeid wamlipe mwombaji maombi ya marejeo ambayo ni Bodi ya Wadhamini ya Klabu ya Yanga," alisema Hakimu Kiswaga.

Wakati huo huo, Rais wa Yanga, Hersi Said, amesema Dube kwa uwezo aliokuwa nao, straika huyo kama hajafikisha mabao 20 basi atakuwa hajafanya vizuri kwenye msimu huu.

Hersi alisema endapo Dube atakuwa fiti na kutokuwa na majeraha yoyote, basi ana uwezo wa kupachika mabao 20 kwa msimu tena na zaidi.

"Dube, ni mchezaji hatari sana, mikimbio yake, harakati zake uwanjani, umaliziaji wake ni hatari sana, ni wa levo nyingine kabisa, mambo ya majeraha ni mipango ya mwenyezi Mungu, mimi nakwambia kama Dube hajafunga chini ya mabao 20 msimu huu Yanga, basi atakuwa hajafanya vizuri. Angalia, mpaka sasa hajaanza kucheza mechi za ligi ameshafunga mabao matatu kama sijakosea na amehusika katika mabao matano katika hizi mechi chache tu ambazo ameshacheza mpaka sasa," Hersi alisema.

***Imeandaliwa na Kulwa Mzee na Adam Fungamwango***

Michezo
Alhamisi Agosti 22, 2024
Nipashe

**Mbappe aifungulia kesi ya madai PSG**

UKURASA 21



# Yanga SC, Magoma watinga Korti Kuu

## ●●●Bodi ya Wadhamini yakata rufani, Dube anadaiwa mabao...

**Na Waandishi Wetu**

WAKATI Bodi ya Wadhamini wa Yanga ikiwasilisha pingamizi Mahakama Kuu Kanda ya Dar es Salaam, ikitaka rufani iliyowasilishwa na Juma Magoma na mwenzake kupinga uamuzi wa Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu itupwe kwa sababu ina makosa ya kisheria, straika mpya wa timu hiyo, Prince Dube, anatakiwa kufunga mabao 20 msimu huu, imefahamika.

Pingamizi hilo liliwasilishwa jana mbele ya Jaji Fatma Maghimbi, wakati shauri hilo lilipokuwa linatajwa.

Katika shauri hilo, Mrufani Magoma na Geofrey Mwaipopo, waliwasilisha rufani wakipinga uamuzi wa Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu uliotupilia mbali mwenendo mzima wa maombi yaliyofunguliwa ya kutaka kuundoa uongozi wa Klabu ya Yanga madarakani.

Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu pia iliamuru Magoma, Mwaipopo na Abeid Mohamed Abeid wamlipe mwombaji (Bodi ya Wadhamini ya Klabu ya Yanga) gharama za uendeshaji shauri hilo.

Baada ya uamuzi huo, Magoma na Mwaipopo kupitia Wakili wao, Jacob Mashenene, waliwasilisha rufani wakiwa na sababu mbalimbali, ikiwamo Mahakama ya Kisutu kutowasikiliza Yanga wakati wa maombi ya kuongezwa muda.

Hoja nyingine ni mahakama iliwapa muda Yanga wa kuwasilisha maombi ya mapitio bila ya kutoa sababu za msingi za kuongezwa muda na sababu ya mwisho ni mwenendo mzima ulikosewa.

Baada ya kuwasilisha hoja hizo za rufani na kuwapa wajibu rufani ambao ni Bodi ya Wadhamini ya Yanga, Fatma Karume, Abeid Abeid na Jabir Katunda, Wakili Kalaghe Rashid, aliwasilisha pingamizi, akitaka rufani hiyo itupiliwe mbali.

Wakili Kalaghe anadai warufani wanakatia rufani uamuzi ambao haukatiwi rufani kisheria na sababu ya pili ni muda umeshapita, hivyo wanaomba ma-

INAENDELEA UK. 23



Kiungo nyota wa Yanga, Pacome Zouazoua, akiwa katika mazoezi kwa ajili ya kujiandaa na mechi ya marudiano ya mashindano ya kimataifa ya Ligi ya Mabingwa Afrika dhidi ya Vital'O itakayochezwa keshokutwa kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam. **PICHA: MTANDAO**

## Simba SC yapeleka 'mashushushu' Libya

**Na Faustine Feliciane**

MABOSI wa Simba tayari wameanza mikakati ya kuhakikisha wanafanya vizuri katika mashindano ya kimataifa ya Kombe la Shirikisho Afrika kwa kutuma 'mashushushu' nchini Libya ili kujipanga kuelekea mechi yao ya hatua ya kwanza ya michuano hiyo.

Timu hiyo ya jiji la Tripoli inatarajia kucheza mchezo wa marudiano dhidi ya Uhamiaji kusaka tiketi ya kusonga mbele kwenye michuano hiyo.

Benchi la ufundi la timu hiyo ambalo liko chini ya Kocha Mkuu, Fadlu Davids, kwa kushirikiana na uongozi wao, wametuma ujumbe maalum ili kuishuhudia Al Ahaly Tripoli ambao huenda wakakutana katika mechi ya hatua ya kwanza ya michuano hiyo.

Ikumbukwe mchezo wa kwanza, Al Ahaly Tripoli iliibuka na ushindi wa mabao 2-0 dhidi ya Uhamiaji na kujiweka katika nafasi nzuri ya kusonga mbele katika michuano hiyo ambapo itakutana na Simba.

Taarifa zilizopatikana jijini zinasema Simba imetuma ujumbe wa watu wawili nchini Libya ili 'kuipeleleza' timu hiyo na kuandaa mikakati ya kuwakabili watakapokutana.

Chanzo hicho kilisema uamuzi wa kuwafuata wapinzani wao umefanya na Fadlu ili kupata taarifa sahihi za wapinzani wao.

"Inaonekana Waarabu hao wa Libya wana nafasi kubwa ya kusonga mbele na kukutana na sisi, benchi la ufundi limetaka kupata taarifa za kina za timu hiyo, ndio sababu ya kutuma wataalamu kwenda kuiangalia na baadaye kutoa ripoti kwa kocha, wana nafasi kubwa ya kukutana na sisi hatua inayofuata," chanzo hicho kilisema.

Yanga, Azam FC zinazoshiriki mashindano ya kimataifa ya Ligi ya Mabingwa Afrika zimeanzia hatua ya awali sawa na Coastal Union ambayo inachuana kwenye michuano ya Kombe la Shirikisho Afrika.

Kwa sasa Simba inaendelea na maandalizi ya mechi yake ya raundi ya pili ya Ligi Kuu Tanzania Bara dhidi ya Fountain Gate FC itakayochezwa Jumapili kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam.

Wekundu hao wa Msimbazi walianza Ligi Kuu Tanzania Bara kwa ushindi wa mabao 3-0, wakiifunga Tabora United kutoka mkoani Tabora, shukrani kwa Che Malone, Valentino Mashaka na Awesu Awesu kwa kupachika mabao hayo.

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >